Mnyama, Joka, Na Mwanamke

Hii ni picha ya kusisimua mno
ya Nguvu mbili zinazoshindana
za wema na uovu
kama zilivyofunuliwa katika Unabii.

Joe Crews

Mhubiri wa Redio ya Amazing Facts

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Orodha Ya Yaliyomo

I. MNYAMA NA HISTORIA 3

Onyo La Kutisha 3
Washindani Wawili Wenye Nguvu 4
Ni Suala La Kufa Na Kupona 5
Ni Mnyama Wa Mfano Tu 7
Dola Nne Za Historia 8
Mnyama Wa Kutisha Wa Nne 9
Pembe Ndogo 10
Utawala Wake Wa Miaka 1260 11
Utimilizo Halisi 11
Mnyama Na Pembe Ndogo Wafanana 13

II. JOKANAMWANAMKE 15

Utabiri Wa Uadui 15
Pande Mbili 16
Joka Na Ibada Ya Jua 16
Mzao Wa Mwanamke 17
JOKA Uzao Wa Joka 18
Madanganyo Katika Vazi La Kipagani 19

III. HESABU NA ALAMA YA MNYAMA 21

Alma Hii ----- Ni Udanganyifu Mkuu 22
Muhuri Wa Mungu 23
Ishara Ya Mamlaka Ya Mungu 24
Muhuri Katika Sheria 24
Muhuri Na Alama Vinashindana 25
Jaribio La Kufanya Mabadiliko 25
Ushuhuda Wa Historia 26
Ukatoliki Unakiri 27
Waprotestanti Wanaafiki 29
Alama Hii Italazimishwa 31

IV. MAREKANI (U.S.A.) KATIKA UNABII 32

Mnyama Wa Pili Atambulishwa 33
Amri Ya Jumapili Kitaifa Iko Karibu 34
Kukata Shauri 35

I. Mnyama Na Historia

Onyo La Kutisha

Onyo la kutisha mno la adhabu linaloweza kupatikana mahali po pote katika Biblia limo katika Ufunuo 14:9,10: "Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa [alama] katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye ATAKUNYWA katika mvinyo ya GHADHABU YA MUNGU iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo."

Maelezo haya yanaogofya mno na hayafanani kabisa na mafungu mengine yanayoielezea tabia ya Mungu ilivyo, hata tunajikunja kwa hofu. Lakini yanaonyesha wazi kipindi kile ambacho rehema ya Mungu itakapoondolewa kwa wale ambao wanaendelea daima kuikataa mamlaka ya mbinguni. Litakuwa ni tendo lisilo na kifani kwa upande wa Mungu katika uhusiano wake na jamii ya kibinadamu. Kwa karibu miaka 6000 hukumu zake za adhabu juu ya watu walio waovu sana zimechanganywa na rehema Yake. Lakini sasa uovu unafikia kiwango ambacho kinafanya iwe lazima kwa Mungu kuingilia kati, na kukidhihirisha kiwango cha usaliti wa mwanadamu dhidi ya Serikali ya Mungu.

Hapa ndipo tunataka kujua habari zaidi juu ya dhambi ile inayomfanya Mungu kutenda tendo hilo la ajabu [geni] la kuwaadhibu [waovu] kwa moto. Angalia kwamba jambo hili la mwisho linahusu utii wa uongo kwa mamlaka ile ya Mnyama, ambayo mara nyingi inatajwa katika unabii wa Biblia. Hatimaye dunia hii itasimama ikiwa imegawanyika katika makambi mawili: Wale wanaomsujudu Mungu wa kweli, na wale wanaomsujudu Mnyama yule wa Ufunuo 13. Lakini ni jambo gani linaloleta mgawanyo huo mkubwa wa watu wa dunia hii? Baada ya kueleza ajali itakayowapata waabudu hao wa uongo katika Ufunuo 14:9-11, Yohana analo hili la kusema katika fungu lile linalofuata: "HAPA NDIPO PENYE SUBIRA YA WATAKATIFU, HAO WAZISHIKAO AMRI ZA MUNGU, NA IMANI YA YESU." Hapa tunaona tofauti ya kushangaza kati ya wale wanaomfuata yule Mnyama na wale wanaomfuata Mwana-Kondoo.

Angalia, tafadhali, ya kwamba suala linalohusika linazunguka juu ya kuzishika amri za Mungu. Wale ambao hawana alama ya Mnyama wanasemwa ya kuwa wanazitii amri hizo [za Mungu], na wale waliobaki wanateseka kwa ghadhabu ya Mungu. Jambo hili linakubaliana kabisa na usemi wa Paulo katika Warumi 16:16, "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki."

Wajibu wa hali ya juu unahesabika kwa tendo hili la UTII. Mwishowe, sehemu kubwa ya wakazi wa dunia hii wataikubali mamlaka hii ya bandia ya serikali ya Mpinga Kristo, kwa KUZIASI AMRI ZILE KUU KUMI za Mungu. Rafiki zangu,

kila mtu mmoja mmoja atakuwa upande mmoja au mwingine. Biblia inaeleza kwa wazi sana ya kwamba UZIMA au MAUTI utategemea UAMUZI WA MWISHO kuhusu Mnyama huyu wa Ufunuo 13.

Ni ajabu kwamba wanathiolojia wa siku hizi wamepuuzia kabisa UJUMBE HUU WA ONYO wa Ufunuo 14, unaohusu ile Alama ya Mnyama. Shauku ya watu wengi imeharibiwa na mvuto wa WACHUNGAJI ambao hawakutaka kuyachukulia maneno haya ya unabii wa Yohana kwa uzito wake. Mara nyingi wanautupilia mbali [unabii huu] kana kwamba ni waraka wenye utata, usiokuwa na maana, ambao ulilihusu tatizo la mahali pale katika kanisa lile la mwanzo. Kwa sababu fulani kitabu hiki kinachoitwa Ufunuo kinahesabika kama vile ni kitabu kilichofungwa [kisichoweza kueleweka], badala ya ukweli wake wa wazi uliofunuliwa [unaoeleweka] kama jina lake linavyomaanisha. Lakini tafadhali zingatia ya kwamba ahadi imetolewa kwa wale wanaoitafuta kweli iliyomo ndani ya kitabu hiki cha ajabu: "Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu." Ufunuo 1:3.

Kabla ya kukichunguza sana kisa hiki kilicho wazi cha Yohana kuhusu pambano lile la mwisho kati ya Kristo na Shetani, hebu na tutumie muda fulani kuwachambua hao wanaopambana katika vita hii. Ni lini na kwa jinsi gani [pambano hili] lilianza, na kwa jinsi gani litafikia mwisho wake?

Washindani Wawili Wenye Nguvu

Japokuwa kilele cha pambano hili kuu kitafikiwa mwishoni kabisa wa historia ya mwanadamu wakati ambapo dunia yote itakuwa imegawanyika katika makambi mawili yanayopingana, pambano hili kati ya Kristo na Shetani limekuwa likiendelea kwa karibu miaka 6000. Lilianza mbinguni kutokana na uasi wa Lusifa dhidi ya utawala wa Mungu wa ulimwengu wote. Kisa cha malaika huyo mzuri aliyetamani cheo cha Mungu Mwenyezi kimefunuliwa katika Maandiko ya manabii kadhaa wa Agano la Kale. Isaya asema hivi kumhusu kiumbe huyo mwenye utukufu: "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri [Lusifa], mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, NITAFANANA NA YEYE ALIYE JUU." Isaya 14:12-14.

Mbegu za uasi wa malaika huyo kiongozi, uliojaa ubinafsi, zikaenea kwa kasi sana na kuathiri utiifu wa malaika wale wengine. Mara hiyo theluthi moja ya jeshi lile la mbinguni ikawa imejiunga na kutoridhika kwa Lusifa, na pambano lile kuu likawa njiani ----- pambano ambalo lingeendelea kwa ukali sana kwa zaidi ya miaka 6000, na ambalo hatimaye lingetaka uamuzi wa kila kiumbe kilicho hai mbinguni na duniani.

Matokeo ya mara moja ya kutopatana yakawa vita mbinguni ambayo ilifikia kilele chake kwa kumfukuza kabisa Lusifa toka mbele zake Mungu na mbele ya malaika wake watiifu. Yohana analieleza jambo hilo kwa njia hii, "Kulikuwa na vita

mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule Joka, yule Joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule Joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote, akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye." Ufunuo 12:7-9.

Malaika yule aliyeanguka hakuweza tena kujulikana kama Lusifa, jina lililomaanisha "nyota ya alfajiri" bali Shetani, likimaanisha "adui." Sasa pambano likawa limehamishwa toka mbinguni na kuja chini duniani. Hapa litaendelea mpaka litakapofikia mwisho wake mbaya sana kwa kuwagawa watu wa dunia hii kuwa upande wa au kinyume na Amri za Mungu. Kama vile pambano hili lilivyoanzishwa kwa uasi dhidi ya mamlaka ya Mungu, ndivyo litakavyokwisha kwa watu kukataa katakata mamlaka Yake yaliyowekwa katika Sheria ya Serikali Yake.

Shetani amekuwapo hapa pamoja na malaika zake waovu tangu wakati ule alipofukuzwa toka kwenye mwanga. Kwa hila yake ya kishetani amefanya majaribio ya njia mbalimbali za kupigana vita dhidi ya Mungu na Mpango wake kwa ulimwengu huu. Kwa kutumia njia mbalimbali za siri zenye kudhuru ameendelea na juhudi zake ili kuipindua mamlaka ya Mungu. Kusudi la kijitabu hiki ni kuonyesha kwa wazi mashambulio yake imara ambayo yamekwisha fanywa, na yanayofanywa na Shetani dhidi ya misingi ya ile Kweli.

Kila kizazi kimeshuhudia onyesho jipya la nguvu ile ya uovu katika vita yake bila kuchoka dhidi ya programu ile ya Mbinguni ya kuuokoa ulimwengu huu. Sura ya mwisho ya upinzani huu wa adui itakuwa ni ile ya Mnyama wa Ufunuo 13. Mamlaka ile ya bandia [uongo] itasimamishwa kupambana vikali sana na Amri za Mungu. Ulimwengu wote utatakiwa KUCHAGUA upande huu au ule. Muungano huo wa [nguvu za] uovu utajiimarisha kwa pambano lile la mwisho linalohusu utii wa wakazi wa ulimwengu huu. Mambo [yote] yatakuwa yamewekwa wazi, na hakuna hata mmoja ambaye hatachagua upande wo wote. UTII KWA MUNGU au KWA SHETANI, kama alivyodhihirishwa katika mamlaka ile ya Mnyama, utakuwa ndiyo nafasi ya pekee kwa mwanadamu ya kuchagua kati ya mambo mawili yaliyo mbele yake.

Ni Suala La Kufa Na Kupona

Sasa, tukiwa tumepata maelezo machache ya kihistoria ya nyuma ya hao wanaopambana, hebu na tuangalie kwa karibu zaidi mpangilio wa Biblia kuhusu pambano hili la mwisho la mkataa [kuamua mshindi ni nani] katika pambano lile kuu [lililoanza mbinguni]. Tafadhali zingatia ya kwamba Mnyama wa Ufunuo 13 anawakilisha mamlaka kubwa sana ya MPINGA KRISTO ambayo inajaribu kumwondoa Mungu kabisa. Hapa pana maelezo ya mamlaka ile katika lugha ya Ufunuo 13:1-7 [Toleo la King James], "Nami nikasimama juu ya mchanga wa bahari, kisha nikaona Mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba [taji] kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru. Na yule Mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha simba, YULE

JOKA AKAMPA NGUVU ZAKE NA KITI CHAKE CHA ENZI NA UWEZO MWINGI. Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia Mnyama yule. Wakamsujudu yule Joka kwa sababu alimpa huyo Mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule Mnyama wakisema, Ni nani afananaye na Mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye? Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru.

Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake MIEZI AROBAINI NA MIWILI. Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa KUFANYA VITA NA WATAKATIFU NA KUWASHINDA, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa."

Hapa hatuwezi kushindwa kuuona ukubwa usio na kifani wa upinzani huu dhidi ya Mungu na dhidi ya wale wanaomfuata. Baadaye katika sura hii hii, tutasoma kwamba mamlaka hii ya Mnyama itakuwa na ushawishi mkubwa sana juu ya dunia nzima, kiasi cha kuwafanya wanadamu kupokea alama [chapa] katika vipaji vya nyuso zao au katika mkono wao [wa kuume]. (Ufunuo 13:16). Mwishoni, wale walio na alama hiyo WATATESWA KWA GHADHABU YA MUNGU ISIYOCHANGANYWA NA MAJI kama ilivyoelezwa katika Ufunuo 14:9,10. Ghadhabu ya Mungu imefafanuliwa zaidi katika Ufunuo 15:1 kwa maneno haya, "Malaika saba wenye MAPIGO SABA YA MWISHO; maana katika hayo GHADHABU YA MUNGU imetimia."

Hali ya kutisha ya mapigo hayo na maumivu makali mno watakayopata wale wanaoipokea chapa [alama] ya Mnyama yamewekwa wazi katika sura ile ya kumi na sita ya Ufunuo. Hatutaongea kirefu juu yake kwa wakati huu, ila na tujikumbushe wenyewe ya kwamba jambo hili litahusu uzima wa milele au mauti kwa wote. Ni kwa bidii ilioje, basi, tungetafuta sana kuelewa Mnyama huyo anawakilisha kitu gani, na jinsi tunavyoweza kuikwepa chapa ile. Pasiwe na kubahatisha au kukisia ko kote juu ya somo hili la maana sana. Yatupasa kujua kabisa hatari iko wapi, na jinsi gani tunaweza kuikwepa.

Mkristo wa kawaida hajapata hata kusikia juu ya umuhimu wa somo hili [kwa maisha yake ya milele]. Hana wazo hata kidogo juu ya Mnyama huyo wala chapa yake, japokuwa maisha yake ya milele yanategemea jambo hilo. Makundi na makundi ya wahubiri wanawafariji watu katika UJINGA wao kuhusu suala hili. Wanasema, "Usiwe na wasiwasi wo wote juu ya Mnyama huyo. Ni jambo gumu sana kulielewa. Mradi tu wewe uzidi kumpenda Bwana utakuwa salama. Huwezi kujua kwa kweli Mnyama huyo ni nani." Sikiliza! Je, Mungu anaweza kutuonya sisi juu ya Mnyama huyo wa kutisha ----- na kisha atuambie ya kwamba haiwezekani kujua huyo ni nani? Je, angeweza kutuambia, "Mtatupwa katika ziwa la moto kama mnayo chapa yake, ila sitawaambia huyo ni nani, ----- ni bahati mbaya sana kwenu kama mnayo [chapa yake]"? La, huyo si Mungu. Yeye anatuonya juu ya hatari ambayo inaweza kuepukwa. Tunaweza tu kujua kwamba sisi tuko salama mbali na Mnyama huyo kama tunamjua Mnyama huyo ni nani. Tunaweza tu kujua kama sisi tumeondokana na chapa [alama] yake kama tunajua chapa yake ni kitu gani.

Ni Mnyama Wa Mfano Tu

Je, yawezekana kujua Chapa [Alama] ya Mnyama huyo ni kitu gani? Twaweza kujua, pasipo kukosea, na ni lazima tujue. Lakini, yatupasa kwanza kuelewa kitambulisho cha Mnyama huyo wa unabii. Hebu na tuweke msingi kwamba Mnyama huyo wa ajabu mwenye tabia kadhaa asichukuliwe kama ni mnyama halisi. Hakuna aliyemwona mnyama aliye na mwili wa chui, kinywa cha simba, na miguu ya dubu. Vitabu vya unabii vya Biblia vinatumia MIFANO na ALAMA (ISHARA). Mnyama huyo anawakilisha kitu fulani. Lakini, je! yeye anawakilisha ishara ya kitu gani hasa? Hapa hatutakiwi kubahatisha. Biblia haiachi mwanya wo wote wa kuwa na mashaka [juu ya jambo hili]. Biblia inajifafanua yenyewe kama komentari ya Mbinguni, nayo inatupatia ufunguo wa kuuelewa unabii wote.

Katika maelezo ya Biblia kuhusu Mnyama huyo kila kitu chake kimewekwa katika mifano. Kwa mfano, fikiria yale maji anamotoka Mnyama huyo. Yanawakilisha nini? Soma jibu katika Ufunuo 17:15, "Kisha akaniambia, Yale MAJI uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni JAMAA na MAKUTANO na MATAIFA na LUGHA." Hakuna uwezekano wa kulikwepa suala hili la msingi juu ya jambo hili. Mungu alieleza kwa wazi maana ya maji katika [lugha ya] unabii. Mara tu mfano mmoja unapotafsiriwa katika unabii uwao wote ule, basi, KANUNI hiyo hutumika katika kila unabii mwingineo. Maji daima yatakuwa mfano wa watu katika lugha hii ya mafumbo ya unabii wa Biblia.

Sasa, namna gani juu ya sehemu nyingine za Mnyama huyo wa ajabu wa kitabu cha Ufunuo? Je, zinawakilisha kitu gani? Ili kumjua Mnyama huyo, yatupasa kurudi nyuma kwenye kitabu kile cha Agano la Kale cha Danieli na kulinganisha Maandiko kwa Maandiko [mengine]. Vitabu vya Danieli na Ufunuo kila kimoja kinakifafanua kingine. Vinapatana kabisa kama mkono na glavu [mpira wa kuvaa mkononi] yake. Zingatia, tafadhali, ya kwamba Danieli alikuwa na maono yanayofanana na yale ya Yohana. Hayo yameelezwa katika Danieli 7:2,3: "Danieli akanena, akisema, Naliona katika maono yangu wakati wa usiku; na tazama, hizo pepo nne za mbinguni zilivuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa. Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini, wote wa aina mbalimbali." Aliyaona maji yale ya unabii kama vile Yohana alivyoyaona, ila Danieli aliwaona wanyama wanne wakitoka baharini [maji mengi] badala ya mmoja tu.

Tumekwisha kuona tayari ya kwamba maji ni mfano wa watu [jamaa] au makutano, lakini, je! wanyama hao wanawakilisha nini? Jibu linapatikana katika fungu la 17, "WANYAMA hao wakubwa walio wanne ni WAFALME wanne watakaotokea duniani." Angalia! Maelezo ni ya wazi kabisa hata hakuna ye yote anayeweza kuuliza swali au kuona mashaka! Mungu anasema kwamba WANYAMA katika unabii wanayawakilisha MATAIFA. Kama vile sisi tulivyo na TAI wa Kimarekani (American Eagle), na Warusi walivyo na DUBU katika msamiati wa kisasa wa masuala ya KISIASA [Tanzania tunaye TWIGA], Mungu naye aliwatumia wanyama zamani, zamani sana kuziwakilisha nchi. Basi, ili kuwa wazi zaidi, Mungu aliongeza maneno haya katika fungu la 23; "Huyo mnyama wa nne atakuwa ni UFALME wa nne juu ya dunia." Kama mnyama yule wa nne anaiwakilisha dola ile ya nne ya historia, basi, wale watatu wa kwanza wangepaswa kuziwakilisha dola zile za kwanza tatu.

Maelezo haya yanarahisishwa zaidi na kueleweka tunapokumbuka kwamba kumekuwa na dola nne tu zilizotawala dunia yote katika historia yote ya dunia hii. Mara kwa mara falme hizo zinatajwa katika unabii wa Biblia na zinatajwa kwa majina yao hasa katika baadhi ya unabii unaohusika katika kitabu cha Danieli. Angalia Danieli 8:20,21 na Danieli 11:2, kama mifano ya maelezo hayo. Katika sura ya pili ya Danieli falme zile zile nne za dunia zinaonyeshwa kwa mfano wa madini nne katika sanamu ile kubwa aliyoiota [Mfalme] Nebukadreza. Dola hizo nne ni BABELI, UMEDI-UAJEMI, UYUNANI na RUMI.

Dola Nne Za Historia

Je, unaweza kuwaangalia kwa karibu zaidi wanyama hao, mmoja mmoja, kama walivyotokea [baharini] katika maono ya nabii yule? Wa kwanza alikuwa "kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai." Danieli 7:4. Hapa tunaona inawakilishwa Dola ile tukufu ya BABELI, ikifananishwa vizuri na yule mfalme wa wanyama [simba]. Ilikuwa ni mojawapo ya dola tajiri kuliko zote, taifa lenye nguvu kuliko yote lililopata kuwamo duniani humu. Angalia kwamba mnyama huyu ana mabawa. Kwa mujibu wa Yeremia 50:44, "MABAWA" katika unabii yanawakilisha KASI [Habakuki l:6-8]. Na kwa hakika, Babeli iliinuka kwa haraka sana na kuchukua nafasi yake kama mtawala wa ulimwengu wote.

Kuanzia 606 K.K. mpaka 538 K.K. Babeli iliendelea kuwa na mamlaka yake yaliyokuwa yameenea kote. Danieli akamwona mnyama wa pili, "kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake." Danieli 7:5. Kwa haraka sana kufuatia nyayo za Babeli ulikuja ufalme wa Umedi-Uajemi mwaka ule wa 538 K.K., hii ni Dola ya ulimwengu ya pili.

Dubu huyo ameinuliwa upande mmoja kuelezea ukweli kwamba Uajemi ilikuwa na nguvu zaidi kuliko Wamedi. Mamlaka zile mbili ziliungana pamoja kuitawala dunia yote. Zile MBAVU tatu huenda zinaonyesha MAJIMBO yale matatu ya ufalme ule ---- BABELI, LYDIA, na MISRI [ambayo waliyateka kwa ukatili].

Kisha katika mwaka ule wa 33l K.K. Umedi-Uajemi iliangushwa chini, na Dola ya tatu ya ulimwengu ikainuka. Kulingana na unabii huu, "[i]kapewa mamlaka." Fungu la 6. Ilikuwa "kama chui, naye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege; mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne." Fungu la 6. Mtoto ye yote wa shule aliyejifunza masomo yake ya HISTORIA YA KALE (Ancient History) kwa makini atajua kwamba UYUNANI [Ugiriki] ilijitokeza kama mtawala wa ulimwengu aliyefuata. Iskanda Mkuu (Alexander the Great) alikuja akitembea kutoka nchi ile ya mashariki [ya kati] akiiweka dunia yote chini ya miguu yake kwa muda mfupi sana.

Mabawa yale manne ya chui yanaonyesha kasi kubwa sana aliyokuwa nayo Iskanda katika kuyashinda mataifa [vitani]. Katika kipindi cha miaka minane alikuwa ameushinda kabisa ulimwengu, na kukaa chini akilia kwa sababu hapakuwa na nchi nyingine zaidi za kuzishinda. Walakini yeye hakuweza kujishinda [kujitawala] mwenyewe; alikufa akiwa kijana wa miaka thelathini na mitatu tu kwa ulevi. Wakati

wa kufa kwake ufalme wake uligawanywa miongoni mwa majenerali wake wakuu wanne, Cassander, Lysimachus, Seleucus, na Ptolemy. Vichwa vinne vya mnyama huyu vinawakilisha mgawanyo huo wa dola yake. Hilo linatufikisha kwenye mwaka wa 168 K.K., na kwenye anguko la Dola ile ya Kiyunani katika mwaka ule ule. Mpaka hapo, maelezo ya kila kitu katika unabii huo yametimizwa kabisa.

Mnyama Wa Kutisha Wa Nne

Hebu sasa na tuangalie kule kutokea kwa mnyama yule wa nne, ambaye ni "ufalme wa nne juu ya dunia." Fungu la 23. Japokuwa Danieli alikuwa amewaona wanyamapori hai kama wale walioonyeshwa katika mifano mitatu ya kwanza ya unabii huu, alikuwa hajapata kuona kitu cho chote kinachofanana na mnyama huyu wa kutisha wa nne. Biblia inamweleza kwa njia hii: "Baadaye nikaona katika njozi ya usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi, naye alikuwa na meno ya chuma, makubwa sana; alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake:... naye alikuwa na pembe kumi." Fungu la 7.

Kama tulivyokwisha kujifunza tayari, huyo anaiwakilisha Dola ile ya nne ya ulimwengu, ambayo ilikuwa ni UFALME WA CHUMA wa Rumi. Kuenea kwa ukatili wa utawala wake ulimwenguni kumeandikwa vizuri, kumbukumbu zake, katika kurasa za historia ya kale. Walakini taifa hili kubwa nalo pia lilikuwa ligawanyike kama fungu la ishirini na nne linavyoonyesha. "Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka WAFALME KUMI." Tafadhali zingatia kwamba hiyo ni tafsiri ya Mungu kuhusu zile pembe kumi zilizokuwa juu ya mnyama huyo. Rumi ilikuwa igawanyike katika sehemu kumi.

Kwa kufuata mkondo wa historia tunagundua ya kwamba kutimizwa kikamilifu [kwa mgawanyo huo] kulitokea katika mwaka ule wa 476 B.K.. Makabila makali sana yalishuka kutoka katika nchi ya kaskazini, na kulishinda eneo [la Rumi] la Ulaya Magharibi, wakiligawa sawasawa katika sehemu zile kumi. Sehemu hizo, kusema kweli, zinahusiana na vidole vile kumi vya sanamu ile kuu ya Danieli 2.

Wanafunzi wote wa historia wanafahamu vizuri sana majina ya makabila yale yaliyoishinda Ulaya Magharibi mwaka 476 B.K.. [Makabila hayo] yalikuwa ni Waanglo-Saksoni (Anglo-Saxons) [Waingereza], Waalemani (Alemanni) [Wajerumani], Waheruli [Heruli], Wavandali (Vandals), Waostrogothi (Ostrogoths), Wavisigothi (Visigoths) [Wahispania], Wasuevi (Suevi)[Wareno], Walombadi (Lombards) [Waitalia], Waswisi (Burgundians) [Switzerland], na Wafaransa [Franks]. Saba kati ya makabila hayo bado yangali yapo mpaka leo hii, yakiwa yamekua na kuwa mataifa ya siku hizi. Bado yanaonekana katika ramani ya Ulaya kama mamlaka zenye nguvu za karne ya ishirini. Matatu kati ya hayo [Waheruli, Wavandali, na Waostrogothi] yalitoweka kabisa katika jukwaa la historia, kama tutakavyojifunza muda mfupi tu ujao.

Pembe Ndogo

Sasa tuko tayari kusoma fungu linalofuata la unabii ule, na kutafuta maana ya pembe ndogo katika maono haya ya Danieli. "Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu." Fungu la 8. Hapa yatupasa kuwa waangalifu sana sana hasa. Yatupasa tusifanye kosa katika kuitambulisha kwa uongo mamlaka hiyo ya pembe ndogo, kwa sababu itajidhihirisha kuwa ni ile mamlaka kuu ya Mpinga Kristo iliyotajwa katika historia.

Ili kuepukana na makosa yote ya kuitambulisha, lingekuwa jambo jema kwetu kufikiria kwanza ishara za tabia yake zipatazo tisa ambazo zimeelezwa katika unabii huu huu. Ishara hizo za kuitambulisha [pembe ndogo] zitatuwezesha kuwa na hakika kabisa na tafsiri yake. Hatudiriki kubahatisha au kukisia kuhusu uthibitisho wa historia wa hiyo "pembe ndogo" ya unabii huu.

KWANZA kabisa, pembe ile ndogo ilizuka [ilitokea] miongoni mwa pembe zile kumi. Jambo hilo linaiweka [pembe ndogo] kijiografia katika eneo la Ulaya Magharibi. PILI, ilizuka "kati yao." Kwa kuwa pembe zile kumi zilitokea mwaka ule wa 476 B.K., pembe ile ndogo ingeanza utawala wake kipindi fulani baada ya mwaka ule. TATU, ingeyang'oa matatu kati ya yale makabila kumi wakati wa kutawala kwake. Fungu lile la nane linasema kwamba mbele yake ile pembe ndogo "pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa."

NNE, pembe ndogo ingekuwa na "macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu." Fungu la 8. Hii inaonyesha kwamba mwanadamu angeiongoza mamlaka hiyo iliyowakilishwa na pembe ndogo. TANO, "Naye atakuwa mbali na hao wa kwanza [wafalme kumi wa kwanza]." Fungu la 24. Hii inamaanisha kwamba pembe ndogo ingekuwa ni mamlaka tofauti na zile falme za kisiasa tu ambazo zilikuwa zimeitangulia. Tabia ya SITA inafunuliwa katika sehemu ya kwanza ya fungu lile la ishirini na tano, "Naye atanena maneno KINYUME chake Aliye juu..." Fungu lingine linasema, "maneno makuu, ya makufuru" Ufunuo 13:5.

Kufikia hapa, labda tungeeleza kwa kutumia Biblia maana ya MAKUFURU. Katika Yohana 10:30-33, Yesu alikuwa karibu kupigwa kwa mawe kwa kudai kuwa Yeye alikuwa UMOJA NA BABA. Wayahudi waliokuwa tayari kumwua walisema, "Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa KUKUFURU, na kwa sababu WEWE ULIYE MWANADAMU WAJIFANYA MWENYEWE U MUNGU." Kulingana na fungu hili ni kukufuru kama mwanadamu akipewa mahali pa Mungu.

Hebu sasa na tusome maana nyingine ya kukufuru. Yesu alikuwa amemsamehe mtu mmoja dhambi zake, na waandishi wale wakasema, "Mbona huyu anasema hivi? ANAKUFURU. Ni

nani anaweza kusamehe dhambi isipokuwa mmoja tu, ndiye Mungu?" Marko 2:7. Ni wazi, Yesu hakukufuru, kwa sababu alikuwa Mungu, alikuwa na uwezo wa kusamehe

dhambi. Lakini kwa MWANADAMU kutoa madai hayo lingekuwa jambo la KUKUFURU, kwa mujibu wa maelezo ya Biblia yenyewe.

Sasa tunakuja kwa ile ishara ya SABA ya kuitambulisha [pembe ndogo], hiyo tunaipata vile vile katika fungu la ishirini na tano, "Naye atawadhoofisha watakatifu Wake Aliye juu." Hilo linaonyesha kwamba pembe ndogo ni mamlaka INAYOTESA watu. Itafanya vita na watu wa Mungu, na kuwafanya WAUAWE. Ishara ya NANE pia inatolewa katika fungu la ishirini na tano, "Naye ataazimu kubadili majira na sheria." Ni wazi, katika upinzani wake mkali dhidi ya Mungu Aliye Mbinguni, kwa kunena maneno makuu dhidi Yake, mamlaka hii pia inatafuta KUIBADILI SHERIA KUU ya Mungu. Kitendo hiki cha pembe ndogo kingeweza tu kuwa JARIBIO (ATTEMPT) la kufanya badiliko hilo. Ni wazi, Sheria ile ya Maadili ya Mungu HAIWEZI KAMWE KUBADILISHWA NA MWANADAMU.

Utawala Wake Wa Miaka 1260

Ishara ya TISA, na ya mwisho ya kuitambulisha [pembe hiyo ndogo], katika fungu la ishirini na tano, hutuambia kabisa kwa muda gani pembe hiyo ndogo ingeyatumia mamlaka yake juu ya dunia hii, "Nao watatiwa mikononi mwake kwa WAKATI, NA NYAKATI MBILI, NA NUSU WAKATI." Hapa tumekabiliwa na usemi wa ajabu. Kwa kweli ni usemi ambao Biblia yenyewe inaufafanua. Katika Ufunuo 12:14, tunasoma maneno haya kuhusu kipindi kile kile cha wakati: "Mwanamke yule akapewa mabawa mawili ya tai yule mkubwa, ili aruke, aende zake nyikani hata mahali pake, hapo alishwapo kwa WAKATI NA NYAKATI NA NUSU WAKATI, mbali na nyoka huyo." Sasa soma fungu la sita, ambalo linalieleza tukio lilo hilo. Badala ya kusema, "wakati na nyakati na nusu wakati," linasema, "siku elfu na mia mbili na sitini." Kwa hiyo tunaona ya kwamba vipindi hivyo viwili vya wakati VINAFANANA KABISA. Kwa kuyalinganisha Maandiko hayo, tunaelewa kwamba wakati mmoja ni mwaka mmoja. Hilo hutupatia nyakati 3 1/2, au miaka 3 1/2, kwa sababu miaka 3 1/2 ni sawasawa kabisa na siku 1260. Naam, tunatumia mwaka wa Biblia ulio na siku 360.

Sasa tuko tayari kutumia KANUNI nyingine kuu ya kutafsiri unabii huu. Tafadhali zingatia siku zote ya kuwa katika kupima wakati wa unabii, Mungu anatumia siku moja kuwakilisha mwaka mmoja. Katika Ezekieli 4:6 tunaisoma kanuni hiyo, "Siku moja kwa mwaka mmoja, nimekuagizia." Kuungwa mkono zaidi tunakupata katika Hesabu 14:34. Njia hii ya kuhesabu wakati ni lazima itumike siku zote katika somo la unabii wa Biblia. Kwa hiyo, hii inamaanisha kwamba mamlaka ya pembe ndogo ingetawala kwa MIAKA 1260, badala ya SIKU l260 tu.

Utimilizo Halisi

Sasa mbele yetu tunayo orodha ya tabia maalum tisa, ambazo zimetolewa toka katika sura ya saba ya Danieli, ili kuifafanua pembe ile ndogo. Kuna mamlaka moja tu

katika historia yote ambayo inapatana kabisa na maelezo yaliyotolewa hapa. Kwa shida mno ishara yo yote katika hizo inaweza kutumika kwa [mamlaka] nyingine, isipokuwa ni UPAPA peke yake. Kanisa Katoliki peke yake linatimiza mambo yote yanayoitambulisha [pembe hiyo ndogo] ambayo yametajwa katika Danieli 7.

Hebu na tuangalie kwa haraka na kuona kwa wazi jinsi jambo hilo linavyotekelezwa. KWANZA kabisa, UPAPA ulitokea [katika eneo la] Ulaya Magharibi, katikati kabisa ya eneo la Dola ya Rumi ya Kipagani ----- katika RUMI yenyewe. PILI, ulizuka baada ya mwaka 476 B.K. wakati Mfalme Justinian alipomteua Papa kuwa mtawala wa KISIASA na wa KIROHO wa ulimwengu wote. Haya ni mambo ya kweli ya historia ambayo yanaweza kuhakikishwa kutoka katika chimbuko la mamlaka yo yote ile ya kihistoria.

TATU, Upapa ulipotokea ulipingwa na makabila matatu ambayo yalikuwa yametawala baada ya kuangushwa kwa Dola ya Kirumi. Wavandali (Vandals), Waostrogothi (Ostrogoths), na Waheruli (Heruli) walikuwa ni mamlaka zenye imani ya Arius (Arian powers) ambao kwa nguvu zao zote walipinga kuzuka kwa Kanisa Katoliki. Majeshi ya Warumi yakayang'oa kabisa na kuyaangamiza makabila hayo matatu. La mwisho katika hayo matatu liliangamizwa katika mwaka ule ule wa 538 B.K., wakati RUMI [YA KIPAPA] ilipoanza kutawala dunia.

NNE, Katika mfumo wake, Kanisa Katoliki lilikuwa na MTU akiliongoza. TANO, Upapa ulikuwa ni UFALME ULIO TOFAUTI na falme zile nyingine za kisiasa zilizoutangulia. Ulikuwa ni MAMLAKA YA KIDINI NA KISERIKALI ambayo iliitawala dunia yote. Hakuna mamlaka iliyofanana kabisa na hiyo ambayo ilipata kuonekana ulimwenguni kabla ya wakati ule.

Sasa tunaiangalia tabia yake ya SITA ----- ile ya kunena maneno makuu na makufuru dhidi yake Aliye juu. Je, Upapa unatimiza maelezo hayo? Tunahitaji tu kukumbushwa kwamba Kanisa Katoliki limejitwalia lenyewe UWEZO WA KUSAMEHE DHAMBI. Kuhusu maneno yake makuu, hebu ninukuu kutoka katika makala ya F. Lucii Ferraris, iliyo katika kitabu cha PROMPTA BIBLIOTHECA CANONICA JURIDICA MORALIS THEOLOGICA. Kitabu hiki kilichapishwa mjini Roma, na kimeidhinishwa na ensaiklopidia ya Kikatoliki. Sikiliza madai haya: "Papa ni mkuu mno, naye ametukuzwa sana, kiasi kwamba yeye si mtu tu, bali kama ilivyo, yeye ni Mungu na Aliye Badala ya Mungu (Vicar of God). Kama ilivyo, PAPA NI MUNGU DUNIANI. Mfalme mkuu wa wafalme, mwenye uwezo mwingi." Gombo la VI, uk.25-29. Haya ni maneno machache tu ambayo Biblia inasema kuwa ni makufuru. UPAPA unatimiza ishara zote za utambulisho na hivyo kuwa ile PEMBE NDOGO.

Sasa tunakuja kwenye kitambulisho cha SABA, tunaona ya kwamba HISTORIA inaunga mkono unabii huu kuhusu MATESO YA PAPA. Kila mmoja anayejua habari za Kizazi kile cha Kati (Middle Ages) [Zama za Giza] anafahamu fika ukweli kwamba mamilioni ya watu waliteswa [kikatili mno] na kuuawa na Mahakama Maalum za Kikatoliki (Inquisitions). Kutoka katika kitabu kilichoandikwa na Kadinali wa Kikatoliki, ambacho pia kimeidhinishwa na Kanisa [Katoliki], tunasoma hivi: "Kanisa Katoliki... lina hofu kuu ya kumwaga damu. Hata hivyo, linapokabiliwa na UZUSHI [HERESY]... LINALAZIMIKA KUTUMIA NGUVU, kutoa adhabu ya kupigwa viboko mwilini, na KUTESA. Linaunda mahakama kama ile ya Inkwizisheni (Inquisition). Linatumia SHERIA ZA SERIKALI kulisaidia... Lilifanya

hivyo hasa katika karne ile ya 16 kuhusiana na WAPROTESTANTI... Katika nchi ya Ufaransa, chini ya [wafalme] Francis I na Henry II, katika nchi ya Uingereza chini ya (Malkia) Mary Tudor, [Kanisa Katoliki] liliwatesa wazushi." Maneno haya yamenukuliwa kutoka katika kitabu cha 'THE CATHOLIC CHURCH, THE RENAISSANCE AND PROTESTANTISM', uk.182-184.

Tunaweza kuongeza semi nyingi kama hiyo kutoka kwa wanahistoria, Wakatoliki na Waprotestanti, zinazoelezea MATESO YA KUTISHA ya mamlaka ya kipapa juu ya Waprotestanti. Kwa njia hiyo tunaweza kuona utimilizo kamili wa maelezo haya ya pembe ndogo. Ishara ya NANE, kama ilivyotolewa katika fungu la ishirini na tano, inahusu jaribio lile la kubadili Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Je, jambo hilo linahusika na Upapa? Tafadhali zingatia haya: Kanisa Katoliki limeondoa Amri ya Pili kutoka katika vitabu vyake vya mafundisho ya dini na Katekisimu zake, kwa sababu inashutumu IBADA YA SANAMU. Kisha Amri ya Kumi imegawanywa [sehemu mbili] ili waendelee kuwa na Amri Kumi. Walakini mbili zinakataza KUTAMANI, na hakuna hata moja inayokataza IBADA YA SANAMU. Kwa njia hii, Upapa UMEAZIMU [UMEFIKIRIA] kubadili Sheria ya Mungu, lakini bila mafanikio. SHERIA YA MUNGU HAIWEZI KUBADILISHWA.

Mwishowe, tunakuja kwenye ishara ile ya TISA ya kitambulisho chake, ambayo inatuambia hasa muda ambao mamlaka hii ya Upapa ingeyatumia mamlaka yake juu ya dunia hii. Tuligundua kwamba ingetawala kwa miaka 1260. Je, jambo hilo linakubaliana na [kumbukumbu za] historia? Kumbuka, ya kwamba tumeona jinsi Upapa ulivyoanza utawala wake, kwa amri ya Justinian, katika mwaka wa 538 B.K.. Tukihesabu kuja upande wetu miaka 1260 kuanzia mwaka huo tunaletwa kwenye mwaka wa 1798. Katika mwaka uo huo Jenerali wa Kifaransa, Berthier, aliongoza majeshi yake kuingia mjini Roma na kumng'oa Papa [Pius wa VI] kutoka kwenye kiti chake cha enzi. Alichukuliwa uhamishoni, na mali zote za Kanisa zikataifishwa [zikanyang'anywa]. Uongozi wa Serikali ya Kifaransa ulitoa amri kwamba pasingekuwa na Askofu mwingine wa Roma kamwe. Kwa kadiri ulimwengu ulivyohusika, na kwa mwonekano wa nje, Kanisa Katoliki lilikuwa limekufa. Baada ya miaka 1260 kamili, kwa kutimiza unabii huu, likapoteza utawala wake juu ya dunia hii. Hivyo pointi hii ya mwisho imetimizwa kwa wazi kabisa katika Upapa, na katika Upapa peke yake.

Mnyama Na Pembe Ndogo Wafanana

Huenda unashangaa kwamba mambo haya yote yana uhusiano gani na Mnyama yule wa Ufunuo 13. Sasa tuko tayari kumtambulisha Mnyama yule mwenye tabia kadhaa aliyeelezwa katika kitabu cha Ufunuo. Hebu na tusome maelezo ya Mnyama huyo kwa mara moja tena, ambaye ana mwili wa chui, miguu ya dubu, na kinywa cha simba. "Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru." Fungu la 5. Angalia, tafadhali, ya kwamba Mnyama huyu anafanya jambo lile lile sawasawa na pembe ile ndogo ya Danieli. Fungu la tano linaendelea kusema hivi: "Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili." Ni muda gani unawakilishwa na miezi arobaini na miwili: Ni siku au miaka 1260 kamili ----- sawasawa na nyakati 3 1/2 za unabii wa Danieli.

Kumhusu Mnyama huyu, tunasoma zaidi maneno haya, "Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda." Fungu la 7. Pia Mnyama huyu ni mamlaka itesayo watu. Kwa maneno mengine, Mnyama wa Ufunuo 13 ni mamlaka ile ile ya pembe ndogo. Wote wawili huuwakilisha Upapa. Hii ni picha [katuni] ya mamlaka ya Upapa kama ilivyotolewa na Mungu, ikionyesha wakati ule [Upapa] ulipotumia mamlaka yake kwa njia ya kidikteta juu ya dunia yote kwa miaka 1260.

Mlandano [kufanana] wa ziada unapatikana kwa kusoma Ufunuo13:3, "Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia Mnyama yule." Kama tulivyokwisha kuthibitisha, jeraha la mauti alipewa mwaka ule wa 1798 B.K., wakati majeshi ya Kifaransa yalipomchukua Papa [Pius wa VI] na kumpeleka uhamishoni [kule Ufaransa]. Lakini jeraha lile lingepona, na mwishowe dunia yote ingetoa UTII wake kwa UPAPA tena. Unabii ule umetimizwa sawasawa kabisa mbele ya macho yetu.

Ulikuwa ni mwaka ule wa 1929 Mussolini alipotekeleza Mapatano (Concordat) yale ya mwaka wa 1929 kati yake na Papa, akimrudishia mali yote iliyokuwa imetwaliwa kutoka mikononi mwa Kanisa. Wakati ule Papa akafanywa kuwa mfalme tena, na Mji Mkuu wa Vatikana (Vatican City) ukaanzishwa kama [makao makuu ya] mamlaka yake ya KISIASA. Tangu siku ile mpaka leo, uwezo wa Upapa umekuwa ukizidi kuongezeka kwa hatua kubwa sana.

Wakati huu wa sasa karibu nchi zote za dunia zinao wawakilishi wao wa kisiasa [mabalozi] katika Mji Mkuu wa Vatikana. Ushawishi usiosadikika wa Upapa katika mambo ya ulimwengu unashuhudiwa katika magazeti ya siku hizi. Karibu kila usemi wa Papa unachapishwa na kusambazwa kwenye miisho ya dunia, na mamilioni kwa mamilioni ya watu wanaitazamia mamlaka hii ya Kipapa kama ni uongozi mkuu mno katika siasa leo. Naam, jeraha limepona hakika, na ulimwengu unaendelea kumfuata Mnyama huyu.

II. Jokanamwanamke

Kufikia hapa tuko tayari kuuliza swali jingine kuhusu kujitwalia mamlaka kwa upande wa Mnyama huyu. Alipokea kwa nani uwezo wa kuitawala dunia kwa miaka ile 1260, na kuwatesa mamilioni [ya watakatifu aliowaita wazushi] kiasi hicho kwa ajili ya imani yao? Jibu linapatikana katika Ufunuo 13:2, "yule Joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi." Angalia ya kwamba MAMLAKA yake inatoka kwa JOKA. Lakini Joka huyu ni nani? Ufunuo 12:7-9: "Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule Joka, yule Joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule Joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye."

Joka ni Shetani mwenyewe hasa. Lakini ni lini Shetani alipoudanganya ulimwengu wote? Alipotupwa chini kutoka mbinguni palikuwa na watu wawili tu duniani, na hao ndio walioiwakilisha dunia yote. Kwa kuwadanganya Adamu na Hawa katika Bustani ile ya Edeni, Shetani aliifanya dunia yote ipotee, naye akaimiliki kwa muda. PAMBANO KUU kati ya mema na mabaya, ambalo lilianza kule mbinguni, sasa likawa limehamia katika sayari hii.

Utabiri Wa Uadui

Baada ya anguko la mwanadamu Mungu alitamka laana juu ya kila mshiriki katika kosa lile la kwanza. Katika Mwanzo 3:15, tunasoma juu ya laana ambayo iliwekwa juu ya Mwovu au Joka. "Nami nitaweka UADUI kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." Hapa kuna unabii wa pambano hili lililodumu kwa vizazi vyote ambalo lingekuwapo kati ya Joka na Mwanamke, kati ya uzao wa Joka na uzao wa Mwanamke.

Lakini Mwanamke huyu aliyetajwa katika unabii huu ni nani? Mwanamke, katika unabii wa Biblia, sikuzote analiwakilisha Kanisa. Katika Yeremia 6:2 tunasoma hivi, "Nimemlinganisha Binti Sayuni na mwanamke aliye mzuri, mwororo." [Tafsiri ya King James Version]. Sayuni ni nani? Isaya 51:16, "na kuuambia Sayuni, Ninyi ni watu wangu." Kwa hiyo, pambano hilo kuu limekuwa likiendelea tangu Edeni. Kumekuwa na pande mbili tu tangu wakati ule mpaka sasa. Joka na wafuasi wake wamejipanga dhidi ya Mungu na wafuasi Wake. Kweli dhidi ya Uongo, na Shetani dhidi ya Kanisa.

Pande Mbili

Shetani na Mungu wamekuwa wakishindania kumtawala kila mwanadamu aliye hai. Hata katika wana wa Adamu pande hizo mbili ziliwakilishwa. Kaini alikuwa upande wa Joka, naye alitaka kuweka njia yake mwenyewe badala ya njia ya Mungu aliyokuwa amemwamuru. Habili alikuwa upande wa Mungu, naye alikuwa mwenye haki sana hata Kaini akamwua hatimaye. Je, unakumbuka Mungu alivyomwambia kila mmoja wao kuleta mwana kondoo, lakini Kaini akaleta matunda na mboga za majani badala ya kile Mungu alichokuwa amewaagiza kuleta kama kafara [dhabihu]? Utagundua kwamba sikuzote hiyo itakuwa ndiyo ALAMA ya Joka. Anajaribu kuweka kitu kingine badala yake au kuleta kitu cha bandia na kukiweka mahali pa kweli halisi ya Mungu.

Katika vizazi vyote vya Kaini dunia ilikuwa imeharibika sana hata Mungu akalazimika kuiangamiza kwa Gharika. Lakini baada ya Gharika pande mbili tena zikaonekana. Wafuasi wa Joka wakakaa kwa wingi katika mji wa Babeli, nao wakajaribu kumchokoza Mungu kwa kujenga mnara mrefu ambao ungefika mbinguni. Kwa kweli mpango ule ulishindikana, na eneo lile la mnara ule wa Babeli baadaye likawa mji wa Babeli (Babylon), ambao, katika mwaka wa 606 K.K. ulianza kutawala kama Dola ya kwanza ya ulimwengu mzima.

Katika miaka ile ya mwanzo ya machafuko Mungu alimwita Ibrahimu kutoka Babeli, na kumtuma Kanaani. Ibrahimu alikuwa amekulia [katika mji ule wa Babeli] kule Mesopotamia, karibu na mahali ambapo mnara ule mrefu wa Babeli ulijaribiwa kujengwa, na mahali ambapo dola ile ya Babeli ilianzishwa. Siku zote mpango wa Mungu umeambatana na mwito wa kujitenga na MACHAFUKO YA UONGO.

Joka Na Ibada Ya Jua

Hebu na tujifunze historia inayohusu upande wa Joka kwa kifupi. Mfumo wa kipagani wa dini ulianzia pale [Babeli] katika mtindo ule wa KUABUDU JUA. Ilikuwa ni ibada ya sanamu ya kumkashifu Mungu, iliyojaa ufisadi, sherehe za ukware [uasherati], na ibada za aibu. Lakini kitambo kidogo tu wafuasi wale wa Joka wakaanza kugombana wao kwa wao na Umedi-Uajemi ikatwaa mamlaka. Ibada ya Baali ikaendelea na kukithiri kama ilivyokuwa katika ufalme uliotangulia. Ndipo Uyunani ikatwaa mamlaka, lakini nayo ikachangia katika kuendeleza ibada iyo hiyo ya jua. Mwishowe, Rumi ikaanza kutawala ulimwengu. Walakini hapakuwa na badiliko lo lote katika dini. Umithra (Mithraism), au IBADA YA JUA, ulikuwa ndiyo dini ya ulimwengu wote wa Dola ile ya Kipagani ya Rumi. Toka Babeli mpaka Rumi, Joka alitawala kwa njia ya ibada ya jua ya kishenzi [kipagani].

Lakini wakati wa utawala wa Warumi, jambo kubwa lilitokea! Ulikuwa ni wakati wa uzao wa mwanamke kutokea! Kumbuka, ya kwamba unabii ulizungumzia juu ya uadui kati ya uzao wa Mwanamke na uzao wa Joka. Uzao wa Mwanamke ulitokea katika siku za Dola ya Kirumi. Hebu na tusome habari zake katika Ufunuo 12:1, "Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini

ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili." Usisahau kwamba Mwanamke katika unabii anawakilisha Kanisa. Mwanamke Safi anawakilisha Kanisa la Kweli [la Mungu], lakini Mwanamke Kahaba anawakilisha mfumo wa Dini ya Uongo [Kanisa lililomwasi Mungu].

Mzao Wa Mwanamke

Mwanamke huyu aliyevaa mavazi meupe, aliyeelezwa katika Ufunuo kumi na mbili, analiwakilisha Kanisa la kweli, Kanisa la Mitume, lenye mafundisho safi ya dini. Nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake ni Mitume wale kumi na wawili. "Naye alikuwa na mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa. Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba [taji] saba. Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake. Naye akazaa mtoto manamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi." Ufunuo 12:2-5. Sasa, basi, mtoto huyo mwanamume alikuwa ni nani? Pamekuwapo na mtoto mwanamume mmoja tu aliyekusudiwa kuyatawala mataifa yote na ambaye alinyakuliwa hata kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Alikuwa si mwingine bali ni Yesu Kristo. Lakini ni nani aliyejaribu kumwua mtoto huyo mara tu baada ya kuzaliwa kwake? Unajibu, Ni Herode, mfalme wa Kirumi." Na hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa. Herode alijaribu kuwaua watoto wote wa kiume katika nchi ile ya Yudea, kwa jitihada ya kumwangamiza Kristo.

Kwa hiyo, Dola ya Kirumi inawakilishwa katika unabii wa Biblia na Joka lile lile kama alivyo Ibilisi mwenyewe. Kwa vile Shetani alifanya kazi yake kwa karibu sana kupitia kwa taifa lile ili kumwangamiza Yesu, Rumi ya Kipagani nayo inawakilishwa na mfano ule ule [wa Joka Jekundu] katika unabii huu kama [anavyowakiliswa] Ibilisi. Walakini Herode hakufanikiwa katika jaribio lake la kumwangamiza mtoto yule mwanamume. Mariamu na Yusufu wakakimbilia Misri na kuokoka kutokana na amri ile ya kutisha. Pigo la kifo la Shetani la kumwangamiza Yesu pale msalabani lilishindwa siku ile ya Jumapili asubuhi wakati Yule Aliyesulibiwa alipovivunja vifungo vya mauti kwa njia ya ufufuo ule. Siku arobaini baadaye alinyakuliwa hata mbinguni kwa utimilizo mkamilifu wa maneno ya unabii huu.

Joka alipoona ya kuwa hakuwa na uwezo wa kumwangamiza Kristo, aligeuza ghadhabu yake dhidi ya Kanisa lile la mwanzo. Kwa mujibu wa Ufunuo 12:13, "Na joka yule alipoona ya kuwa ametupwa katika nchi, alimwudhi [alimtesa] mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume." Wakati ule ilikuwapo idadi ndogo tu ya Wakristo katika ulimwengu wote, na Shetani alijisikia ya kwamba angeweza kuwafutilia mbali kabisa kwa mateso. Maelfu kwa maelfu ya Wakristo waliuawa chini ya mateso yale ya kutisha yaliyoendeshwa na Wafalme wakatili wa Kirumi. Lakini Injili ilizidi kukua na kuenea mahali pengi. Damu ya wafia dini wale ilionekana kuwa ni mbegu ya Kanisa. Alipokufa mmoja waliinuka mia moja zaidi kuijaza nafasi yake. Paulo alihubiri Injili yake mpaka milangoni mwa Rumi. Joka

yule wa zamani akaingiwa na wasiwasi. Huo haukuwa ni wakati unaofaa kwa uzao wa Joka kuonekana.

JOKA Uzao Wa Joka

Kwa karne nyingi Shetani alijitahidi kuwaangamiza watu wa Mungu kwa kutumia upinzani wa kikatili wa Babeli, Umedi-Uajemi, Uyunani, na Rumi. Kwa njia ya ukatili sana na mateso alikuwa ameshindwa kuifutilia mbali ile kweli [Neno la Mungu]. Basi, kile alichokuwa hana uwezo kufanya kwa kutumia nguvu, Joka sasa angejaribu kufanya kwa kutumia mbinu na udanganyifu. Angeanzisha MFUMO WAKE WA DINI BANDIA[YA UONGO]. Angeingiza mafundisho ya dini ya kipagani na falsafa kutoka katika Dola zile za zamani za Babeli, Umedi-Uajemi, Uyunani na Rumi, na kuyachanganya pamoja na mafundisho ya dini ya Kikristo. Kwa njia hiyo, alijitahidi kuwaangamiza mamilioni kwa udanganyifu wake.

Katika umbile gani uzao huu wa Joka ulitokea? Uliletwa kwa mfano wa Mnyama yule wa Ufunuo 13. Ni jambo la maana sana ya kwamba Mnyama huyo ameumbwa kwa sehemu za simba, chui, dubu, na mnyama wa kutisha asiyekuwa na jina wa Danieli 7. Picha [katuni] hii ya UPAPA aliyoitoa Mungu inatudhihirishia ya kuwa [Mnyama huyo] aliumbwa kwa sehemu zinazotokana na falme zile zote za zamani za kipagani. Hasa alipata nguvu zake kutoka kwa taifa lile la kipagani la Rumi. Kwa mujibu wa Ufunuo 13:2, Joka alimpa Mnyama huyo nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi. Tumejifunza ya kwamba Joka huyo anaiwakilisha hasa Dola ya Kipagani ya Rumi, pamoja na kumwakilisha Shetani mwenyewe.

Je, Dola ya Kipagani ya Rumi ilipata kuupa mamlaka yo yote Upapa? Ukweli ni huu, kwamba katika mwaka ule wa 330 B.K. Konstantino (Constantine), Mfalme wa Rumi, aliukabidhi mji wote wa Rumi kwa Papa kama kiti chake cha enzi. Historia inatumia karibu maneno yale yale ya unabii huu katika kukielezea kitendo hicho. Nitanukuu kutoka kwenye chanzo kimoja cha Kikatoliki na kutoka katika kitabu kimoja cha historia. "Dola ya Rumi ilipogeuka na kuwa ya Kikristo, na amani ilipohakikishwa mfalme [Konstantino] aliiacha Rumi mikononi mwa Papa, kuwa kiti cha mamlaka yake yule Aliye Badala ya Kristo (Vicar of Christ), ambaye angetawala mle akiwa haingiliwi na mamlaka yo yote ya kibinadamu, mpaka mwisho wa dahari, mpaka mwisho wa wakati." PAPAL RIGHTS AND PRIVILEGES, uk.13,14.

"Uhamishaji wa makao makuu ya dola kutoka Rumi kwenda Konstantinopo (Constantinople) katika mwaka ule wa 330 B.K., uliliacha Kanisa lile la Magharibi [Upapa] kuwa huru kabisa mbali na mamlaka yo yote ya kifalme, kuuendeleza mfumo wake wa utawala. Askofu wa Rumi [Papa], akiwa amekikalia kiti chake cha enzi cha Makaisari, kwa sasa akawa mtu mkubwa sana katika eneo la [Ulaya] Magharibi, na kitambo kidogo tu baadaye akalazimika kuwa KIONGOZI WA KISIASA na pia kuwa KIONGOZI WA KIROHO." THE RISE OF THE MEDIEVAL CHURCH, ukurasa 168. Ni kwa wazi jinsi gani semi hizi [mbili] huonyesha kwamba Upapa ulipokea kiti chake cha enzi na uwezo kutoka kwa Rumi ya Kipagani! Lakini Rumi iliupata wapi? Toka kwa Uyunani. Na Uyunani iliupata wapi uwezo wake? Toka kwa Umedi-Uajemi. Na Umedi-Uajemi iliupata wake wapi? Toka kwa Babeli. Na Babeli

iliupata wapi? Toka kwa yule Joka. Basi, tunaanza kuelewa kwa nini Mungu ametoa maonyo ya kutisha kama hayo dhidi ya mamlaka hii ya Mnyama. Joka yuko nyuma yake kabisa.

Madanganyo Katika Vazi La Kipagani

Hebu na tutafakari kwa dakika chache jinsi mafundisho ya dini ya kipagani yalivyoweza kupata nafasi ya kuingia katika mfumo huo wa dini ya bandia [uongo] ambayo Shetani aliianzisha. Kwa sababu dalili ya uwezo wa Joka ni kudanganya kwa KUIGIZA na kuweka kitu kingine mahali pa kile kilichokuwapo, basi, tutaweza kuona katika mfumo huo wa KIDINI-KISIASA utendaji wake Shetani akitumia juhudi yake yote ya kishetani. Kama ilivyokuwa katika suala lile la Kaini, vitu vya badala viliwekwa [mahali pa vyenyewe] ili kutimiza amri za Mungu. Kumbukumbu (relics) nyingi za ibada ya jua zilikuja kupewa cheo cha Kikristo. Seti nzima ya mafundisho ya uongo iliongezwa ili Upapa uweze kupata fahari kubwa kwa watu wale wapagani wa kizazi kile. Sanamu za kipagani zikaachwa mlangoni [mwa kanisa], lakini sanamu za Petro, Maria na watakatifu zikachukua mahali pao.

Kama kielelezo hai cha njia zilizofanya dhana za kipagani kuingia kanisani, hebu fikiria mfano wa Krismasi. Je, unajua usherehekeaji wa Krismasi ulikoanzia? Krismasi, kama sikukuu, ilikuwako muda mrefu sana kabla ya Yesu kuzaliwa duniani humu. Desemba ishirini na tano, kwa kweli, ilisherehekewa mamia ya miaka kabla ya kuzaliwa Kristo. Wapagani waliliabudu jua, nao wakagundua ya kwamba katika mwezi ule wa Desemba siku zilikuwa zinazidi kuwa fupi na fupi zaidi, na jua lilikuwa linakwenda mbali sana kutoka kwao. Wakiwa wamejawa na hofu kwamba jua lingeweza kuwaacha kabisa, wakaanza kusali na kutoa sadaka. Kisha tarehe ishirini na tano Desemba, kwa mara ya kwanza, waliweza kujua ya kwamba jua lilikuwa linarudi kwao kwa karibu zaidi; siku zilikuwa zinaanza kuwa ndefu tena. Basi, watu hao wakasema, "Jua limezaliwa upya kwetu." Wakaiita tarehe ishirini na tano ya Desemba kuwa ni SIKU YA KUZALIWA JUA, ama MUNGU-JUA. Ikawa ni SIKUKUU KUBWA SANA ya kidini kwao.

Siku ile ilisherehekewa na wapagani peke yao mpaka mfumo huo bandia wa Upapa ulipoanza kujitokeza. Wakati ule siku ile ikachaguliwa na Upapa na kuanza kutumika, nayo ikaitwa SIKU YA KUZALIWA MWANA (S-O-N), badala ya SIKU YA KUZALIWA JUA (S-U-N). Dkt. Gilbert Murray, M.A., D. Litt., LL.D., F.B.A., profesa wa Lugha ya Kigiriki katika Chuo Kikuu cha Oxford, ameandika haya: "Umithra (Mithraism) ulikubalika sana, hata ukaweza kuulazimisha ulimwengu ule wa Kikristo kuweka siku yake ya jua (Sun-day) mahali pa [siku ya] Sabato; na sikukuu yake ya kuzaliwa jua, tarehe 25 Desemba, kuwa ndiyo siku ya kuzaliwa Yesu." HISTORY OF CHRISTIANITY IN THE LIGHT OF MODERN KNOWLEDGE, Sura ya III; yamedondolewa kutoka katika kitabu cha "RELIGION AND PHILOSOPHY," uk.73,74. New York: 1929.

Kwa kweli, hatuijui tarehe ya kuzaliwa kwake Kristo. Kama unavyoweza kuona bila shida, kuitumia tarehe ishirini na tano ya Desemba kulijengwa kabisa juu ya maadhimisho ya sikukuu ile ya kuabudu jua. Tafadhali zingatia jinsi siku hii

iliyowekwa na wapagani inavyoweza kuteleza kirahisi na kuingia katika makanisa ya Kikristo, na hata inaweza kurithiwa [kupokewa] na Uprotestanti.

Ni vipi kuhusu Pasaka (Easter)? Ni sherehe inayojulikana sana ambayo inaadhimishwa na makanisa yetu ya siku hizi. Walakini hii pia ilisherehekewa na wapagani muda mrefu kabla ya ufufuo wa Kristo. Makundi yote ya Wakristo wanagundua kwamba Jumapili ya Pasaka mara nyingi inahitilafiana kwa umbali wa majuma matano toka mwaka mmoja kwenda mwaka mwingine. Wachache wanajua kwamba inatawaliwa na mianga ile ya mbinguni. Siku zote Pasaka inaangukia Jumapili ya kwanza baada ya mwezi mpevu (full moon) mara tu baada ya jua kuwa kichwani kaskazini ya Ikweta (Equinox ----- March 2l).

Wapagani wale wa zamani za kale waligundua ya kwamba kila kitu kilionekana kupata uzima mpya mapema katika majira yale ya kuchipua (Spring), mara tu baada ya jua kupita mstari wa ikwinoksi (equinox) kaskazini ya Ikweta. Basi wakachagua siku moja katika majira ya kuchipua [Machi, Aprili, Mei] ili kumheshimu mungu wa kike wa uzazi. Siku ile ikatolewa kwa ISHTA (ISHTAR), mungu wa kike wa uzazi, kwa sababu ya uhai mpya na kukua kwa mimea ya asili. Neno lilo hilo ISTA (EASTER) limeandikwa kwa herufi nyingine zisizokuwa za lugha yenyewe kutokana na jina la mungu huyo wa kike ISHTA (ISHTAR), ambaye ibada yake iliwekewa ukumbusho wake kwa kutumia sikukuu ya Ista (Easter) [Pasaka].

Mara nyingi Wakristo walei [wa kawaida] wameuliza ya kwamba ule mkate mdogo kama sungura (bunny rabbit) na yai la Ista (Easter egg) vina uhusiano gani na ufufuo wa Kristo. Kusema kweli, havina uhusiano wo wote na [ufufuo] huo. Sungura alichaguliwa kwa sababu alikuwa anazaa sana. Yai pia lilichaguliwa kwa sababu lilikuwa nembo ya kuzaa sana. Hata nembo hizo zenyewe, mkate mdogo kama sungura na mayai, vinatunzwa kama ukumbusho wa asili yake ya kipagani [ya siku hiyo]. Mifano hii imetolewa ili kuonyesha tu jinsi ilivyokuwa rahisi kwa Mwovu kulazimisha mawazo yale ya kipagani juu ya kanisa lile. Upapa ulipotokea ulikuwa uko tayari kuzipokea desturi zile zisizoungwa mkono na Biblia ambazo ziliashiria kwa wazi ya kwamba [mfumo] huo ulikuwa ndiyo ile mamlaka kuu ya bandia iliyoelezwa na Mungu katika Ufunuo 13.

Kufikia hapa swali linakuja mawazoni mwetu, ----- Hivi ni kweli tunaifuata Biblia katika mafundisho yetu yote ya dini? Iwapo MAPOKEO na DESTURI za kipagani zimeweza kuteleza kwa urahisi na kuingia kanisani, ni vipi kuhusu mafundisho mengine ya dini? Mpaka sasa mambo yaliyokwisha kutajwa tayari hayapingani na Amri za Mungu moja kwa moja. Hatuna amri yo yote kuhusu uadhimishaji wa ufufuo au kuzaliwa kwa Kristo. Tunaweza kutafakari juu ya ufufuo Wake na kuzaliwa Kwake kwa wakati wo wote ule na katika siku yo yote ile ya mwaka. Katika sura inayofuata tutagundua kwamba mafundisho mengine ya kipagani yaliingizwa [kanisani] ambayo yanaondoa moyo wa dini ile ya kweli ya Biblia. Hatuyashughulikii sana [mambo hayo], isipokuwa mambo yale tu yanayokiuka amri ya wazi ya Mungu.

Mamlaka ya Upapa iliyokuwa inakua iliendelea na programu yake ya kuweka mafundisho mengine ya uongo kinyume na kweli zile zilizomo katika Neno la Mungu. Macho yetu na yafumbuke ili tupate kuyatambua mafundisho hayo ya uongo na kuendelea kuwa watiifu kwa ile kweli halisi katika mfumo wake wa asili.

III. Hesabu Na Alama Ya Mnyama

Mambo mawili makuu sana ya mamlaka hii ya Mnyama yanafunuliwa katika Ufunuo 13. "Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe CHAPA [ALAMA] katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa [alama] ile, yaani, jina la Mnyama yule, au hesabu ya jina lake. Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya Mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita." Ufunuo 13:16-18. Mpaka hapa katika somo letu tumezieleza ishara zile tisa za kuitambulisha mamlaka hii ya Mnyama na kuzitumia kwa Upapa. Hapa tutaongeza pointi ya KUMI katika orodha yetu kwa ajili ya kuifafanua hesabu hii ya jina lake.

Kwa mujibu wa Ufunuo 13:17, hesabu ya jina lake itakuwa pia ni hesabu ya mwanadamu. Bila shaka inamhusu mtu yule anayeiongoza mamlaka ile ya Mnyama. Njia ya zamani ya kuipata hesabu ya jina ni kuchukua thamani ya tarakimu za herufi zote na kuzijumlisha ili kupata jumla yake. Kama tunataka kutumia kipimo hicho kwa Upapa, yatupasa kupata jina la kiofisi [cheo] la Papa, ambaye ndiye kiongozi wa Kanisa hilo. Kama hiyo ni hesabu ya mtu, basi, bila shaka ingekuwa ni ya mtu yule anayeuongoza mfumo ule [wa dini].

Ni jambo la kuvutia macho kuona kwamba kuna cheo rasmi cha Kilatini cha Papa, cheo ambacho amepewa na Kanisa lenyewe. Cheo hicho kinaonekana tena na tena katika vitabu vya Kanisa la Roma. Lakini katika gazeti la kila juma la Kikatoliki liitwalo, OUR SUNDAY VISITOR, la Aprili, 1915, tunao usemi wa kuvutia unaosema kwamba herufi ya cheo hicho rasmi zimeandikwa katika kofia yake ya Kiaskofu (miter or mitre). Hapa ni dondoo lenyewe: "Herufi zilizoandikwa katika kofia ya Papa ni hizi; VICARIUS FILII DEI, ambacho ni Kilatini cha 'ALIYE BADALA YA MWANA WA MUNGU' (VICAR OF THE SON OF GOD). Wakatoliki wanashikilia [wanaamini] kwamba Kanisa ambalo ni jamii inayoonekana ni lazima liwe na kichwa kinachoonekana; Kristo kabla ya kupaa kwake kwenda mbinguni, alimchagua Mtakatifu Petro kuwa kama Mwakilishi wake. Kwa hiyo, Askofu wa Rumi kama kichwa cha Kanisa, alipewa cheo cha 'Aliye Badala ya Kristo' (Vicar of Christ)." Kwa siku hizi kofia ya papa [tiara] haina cheo chake cha Kilatini, lakini maneno hayo yanatumika katika sherehe za kumtawaza kila Papa mpya anayevikwa taji [kofia hiyo].

Basi, tukiwa na cheo hiki rasmi cha Papa mkononi mwetu, tunaweza kuendelea kutumia kipimo hiki cha Maandiko haya. Tunaipataje hesabu ya jina lake? Kwa kupata thamani ya tarakimu za Kirumi za cheo chake cha VICARIUS FILII DEI, tunaifikia hasa hesabu hiyo halisi, 666. Angalia jinsi hesabu hizo zilivyofanywa hapa chini, kila herufi ikipewa thamani ya tarakimu yake:

V 5	F 0	D 500
I..... 1	I 1	E..... 0
C 100	L 50	I .....____1
A 0	I 1	**501**
R 0	I .....____1	
I 1	**53**	
U au V..... 5		
S .....____0		
112		

112 + 53 + 501 = 666

Mmoja anaweza kubisha kwamba hilo linaweza kuwa ni jambo linaloweza kutokea kwa nasibu. Tunakubali ya kwamba upo uwezekano kwa jambo kama hilo kutokea kwa nasibu tu, kama tungekuwa na pointi moja hiyo tu ya utambulisho ya kuitegemea. Lakini, basi, ukweli ni kwamba, hiyo ni pointi ya KUMI miongoni mwa orodha ndefu ya ishara za tabia yake ambazo Biblia huzitumia kuitambulisha mamlaka hiyo ya Mnyama. Hii inaongezea tu uzito na nguvu kwa yale ambayo tayari yamekwisha kusemwa kwa kuzitumia [ishara zile] kuionyesha mamlaka hiyo ya Papa. Ni uthibitisho wa kilele pamoja na zile ishara nyingine zote zilizowekwa kwa wazi sana katika Maandiko.

Alma Hii ----- Ni Udanganyifu Mkuu

Sasa tuko tayari kuchukua hitimisho la kilele cha udanganyifu huu kwa kadiri mamlaka hiyo ya Mnyama huyo inavyohusika. Tayari tumekwisha jifunza ya kwamba mamlaka hii ingeweka mafundisho mengi ya uongo kinyume na mafundisho makuu ya kweli zake Mungu. Kwamba [mamlaka hiyo] ilikuwa ni mchanganyiko wa mawazo ya kipagani na mafundisho ya dini ya Kikristo ambayo yamekusanywa pamoja kwa hali inayoleta machafuko [kuchanganyikiwa], yanayoitwa vyema kama "BABELI" katika Maandiko.

Mafundisho machache ya uongo yanaweza kuorodheshwa kama ifuatavyo: badala ya Neno la Mungu, imeweka MAPOKEO; badala ya Roho Mtakatifu, imemweka PAPA; badala ya toleo moja tu la Kristo, imeweka MISA [toleo la kila siku]; badala ya ubatizo, imeweka KUNYUNYIZA; badala ya Meza ya Bwana, imeweka MKATE UNAOBADILIKA KABISA NA KUWA MWILI NA DAMU HALISI YA YESU (Transubstantiation); badala ya Sheria ya milele ya Mungu, imeweka SHERIA ILIYOFANYIWA MAREKEBISHO [Amri Kumi]; badala ya Zaka; imeweka KODI [Ushuru] na INDULGENSIA [kuuza vyeti vya msamaha wa dhambi]; badala ya mauti, imeweka MAHALI PA KUTAKASIA DHAMBI au TOHARANI (Purgatory); badala ya Muhuri wa Mungu, imeweka ALAMA [CHAPA] YA MNYAMA.

Hapa tunashughulika hasa na ALAMA YA MNYAMA. Katika Ufunuo 14:9,10 tunasoma hivi, "Mtu awaye yote akimsujudu huyo Mnyama na Sanamu yake, na kuipokea chapa [alama] katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake." Hili ni jambo la KUFA NA

KUPONA. Ni lazima tujue kabisa alama hii ni ya kitu gani hasa na jinsi tunavyoweza kuikwepa.

Kwanza tunaona katika Biblia ya kwamba ALAMA hii daima iko kinyume na MUHURI WA MUNGU. Katika Ufunuo 7:2,3, tunajifunza ya kwamba Muhuri wa Mungu unawekwa juu ya kipaji cha uso sawasawa tu na ile Alama ya Mnyama inavyowekwa juu ya vipaji vya uso. Vitu hivyo viwili [Muhuri wa Mungu na Alama ya Mnyama] vinaonekana kuhitilafiana moja kwa moja na kila kimoja kiko kinyume na kile kingine. Vyote viwili vinapokewa katika kipaji cha uso na mkononi. Sasa tutauliza swali, "Je, Muhuri ni kitu gani?" Kama tutalithibitisha jambo hili, basi, litatusaidia kuitambua Alama [ya Mnyama].

Muhuri Wa Mungu

Muhuri ni kitu fulani kinachohusika na mambo ya kisheria. Hati za kiserikali zikuzote zinapigwa muhuri wa mamlaka inayotawala. Kila Serikali inao muhuri ambao unagongwa katika hati zake za kisheria. Kusudi lake ni kuonyesha kwamba kuna mamlaka inayohusika nyuma ya hati ile. Hii ni kweli hasa kuhusiana na sheria za nchi. Kila sheria mpya ina muhuri kuonyesha ya kwamba nyuma yake kuna uwezo na mamlaka kuiunga mkono Sheria hiyo.

Zingatia kwamba kila muhuri una mambo matatu ndani yake. Hauna budi kuwa na JINA la mwenye mamlaka, OFISI au CHEO cha mwenye mamlaka, na ENEO analotawala. Muhuri wa Rais wa Amerika una maneno yafuatayo: Richard M. Nixon, Rais [l977], Marekani (U.S.A.). Muhuri ule unapowekwa juu ya sheria au hati ya Serikali, huonyesha kwamba mamlaka ya Rais inaunga mkono tangazo lile.

Je, Muhuri wa Mungu unahusika na Sheria Yake pia? Kama ndivyo, kwa jinsi gani na wapi unawekwa? Hebu na tusome Isaya 8:16, "Ufunge huo ushuhuda, UKAITIE MUHURI SHERIA kati ya wanafunzi wangu." Hii inathibitisha kwamba muhuri huo unahusiana na sheria. Kwa kweli, Sheria inatiwa muhuri kati ya wanafunzi wa Mungu. Lakini, je! ni wapi inapowekwa hasa Sheria hiyo kwa wale walio waaminifu? Jibu linapatikana katika Waebrania 10:16, "Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana, Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, Na katika nia zao nitaziandika."

Basi, hivyo ndivyo muhuri wa Bwana unavyotiwa juu ya wanafunzi Wake. Unaandikwa mioyoni mwao ama, kwa mfano, juu ya vipaji vya nyuso zao. Mithali 7:2,3 inaliweka jambo hilo wazi zaidi, "Uzishike amri zangu ukaishi, Na sheria yangu kama mboni ya jicho lako. Zifunge katika vidole vyako; Ziandike juu ya kibao cha moyo wako." Unaona ya kwamba sheria hiyo inashikwa kwa mkono na kwa moyo; hivyo, inanenwa kwamba inatiwa mkononi na juu ya kipaji cha uso.

Ishara Ya Mamlaka Ya Mungu

Tunataka kuchunguza katika Sheria ya Mungu kuona ni sehemu ipi hasa iliyo na Muhuri huo. Lakini, kwanza, hebu na tutafute ni kitu gani kinachoonyesha Uweza wa Mamlaka ya Mungu. Rais anayatumia mamlaka yake kwa ajili ya Cheo chake kama Rais. Mungu anadai Uweza wake kutegemea Cheo chake kama MUUMBAJI wa ulimwengu. Angalia maneno haya yanayopatikana katika Yeremia 10:10,11. "Bali BWANA ndiye Mungu wa kweli; Ndiye Mungu aliye hai, Mfalme wa milele; ... Mtawaambia hivi, Miungu hiyo isiyofanya mbingu na nchi, hiyo itaangamia katika nchi, nayo itatoweka chini ya mbingu. Ameiumba dunia kwa Uweza Wake." Tena, katika Zaburi 96:5, "Maana miungu yote ya watu si kitu, Lakini BWANA ndiye aliyezifanya mbingu." Weka pamoja na mafungu haya fungu moja zaidi linalopatikana katika Isaya 40:25,26, "Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa naye? asema yeye aliye Mtakatifu. Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi?"

Tunashawishika kuona kwamba kitu kikuu kinachomtofautisha Mungu wa kweli ni Uweza wake wa Uumbaji. Anajenga madai ya mamlaka yake kama Mungu wa kweli na wa pekee juu ya UWEZA WAKE WA KUUMBA. Lakini, je, ishara au kumbukumbu ya Uumbaji Wake ni ipi? Mwanzo 2:2,3 inatoa jibu: "Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya." SABATO ni kumbukumbu ya uweza wa uumbaji wake ambao unamtofautisha [Mungu] na miungu ya uongo.

Muhuri Katika Sheria

Sasa tuko tayari kuichunguza Sheria ya Mungu ili kuutafuta Muhuri wa Mamlaka Yake na kujua ni kitu gani hasa. Kumbukeni ya kwamba muhuri ni lazima uwe na JINA, CHEO, na ENEO LA UTAWALA. Tunaichunguza amri moja moja katika zile Amri Kumi za Sheria ya Mungu. Kwa taratibu zinaisha zote kasoro moja. Masharti yale matatu ya muhuri yatapatikana tu katika [amri] ile iliyo na Jina, Cheo, na Eneo la Mungu [analotawala].

Katikati kabisa ya Sheria hii ipo kumbukumbu ya Uweza Wake wa Uumbaji, na tazama, katika amri ile ya NNE tunaziona sehemu tatu za muhuri. "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako. (Jina [BWANA= YEHOVA]) ... Maana, kwa siku sita BWANA ALIFANYA (Cheo - MUUMBAJI) mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo (Eneo analotawala), akastarehe siku ya saba." Kutoka 20:8-11. Kwa maneno mengine, SABATO NI MUHURI WA MUNGU ----- ALAMA ya Mmoja pekee awezaye kuumba na ambaye amepewa mamlaka ya kuitawala nchi hii. Tena ili kuifanya Sheria hiyo iwe na nguvu, ameweka Muhuri ndani yake, kuonyesha kwamba

Yeye [Mungu] anasimama nyuma ya kila amri moja moja katika Sheria hiyo [ya Amri Kumi].

Waweza kuuliza, "Je, hivi Sabato ni Muhuri wa Mungu kweli?" Hebu na tuangalie katika Ezekieli 20:12. "Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ISHARA kati ya Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, BWANA, ndimi niwatakasaye." Hapa Sabato inaitwa "ISHARA" ya Mungu. Je, [ishara] hiyo ni sawasawa na muhuri? Warumi 4:11 hufunua kwamba "MUHURI" na "ISHARA" ni kitu kile kile kimoja, maneno hayo hutumika kwa kubadilishana. "Naye aliipokea DALILI [ISHARA] hii ya kutahiriwa, MUHURI wa ile haki ya imani aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa."

Muhuri Na Alama Vinashindana

Hebu na tuone ni uhusiano gani upo kati ya MUHURI WA MUNGU na ALAMA YA MNYAMA. Vitu hivyo viwili vinashindana. Katika Ufunuo 14:9,10, Ujumbe wa Malaika wa Tatu unawafunua wale walio na alama [chapa] hiyo: "Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo Mnyama na Sanamu yake, na kuipokea chapa [alama] katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo."

Katika fungu la kumi na mbili tunalo kundi jingine linalotambulishwa kwa maneno haya, "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu." Kwa maneno mengine, wale WANAOZISHIKA AMRI [KUMI] ZA MUNGU hawana Alama ya Mnyama na wale walio na Alama ya Mnyama HAWAZITII AMRI [KUMI] ZA MUNGU [Yakobo 2:10-12; Kutoka 20:3-17]. Amri hizo Kumi, zilizo na Muhuri wa Mungu, zinawekwa katika mashindano na Alama ya Mnyama. MUHURI ni SABATO, kwa hiyo SABATO ni kinyume na ALAMA hiyo [ya Mnyama]. Basi, je! alama hiyo ni nini?

Jaribio La Kufanya Mabadiliko

Kulijibu swali hilo [juu] tunaelekezwa nyuma tena kwa Danieli 7:25, ambako Upapa unaelezwa kuwa ni mamlaka ile itakayo"azimu kubadili majira na Sheria." Tumekwisha jifunza tayari jinsi amri ya pili ilivyoondolewa na jinsi amri ya kumi ilivyogawanywa katika sehemu mbili katika Katekisimu za Upapa. Lakini, je! ni vipi kuhusu "majira" yaliyotajwa katika Sheria hiyo? Ni katika Amri ile ya Nne. Je, Upapa uliazimu [ulifikiria] kubadili Sabato, ambayo ni majira pekee yaliyowekwa katika Sheria hiyo? Ndio, ulifanya hivyo, na jambo hilo lilitokea kwa njia ya kushangaza.

Wapagani walikuwa na mfumo wao wa dini uliojengwa juu ya ibada ya sanamu. Siku yao takatifu ilikuwa ni siku ile ya kwanza ya juma, ambayo iliitwa Siku ya Jua (Sun-

day) kwa heshima ya Mungu-jua. JUMAPILI [SUNDAY] iliadhimishwa na wapagani kinyume na uadhimishaji wa SABATO kwa Wakristo. Lakini katika siku za Mfalme wa Rumi, Konstantino, jambo kubwa lilitokea. Konstantino alidai kwamba yeye alikuwa ameongoka na kuwa Mkristo, naye akaifungua wazi milango ya Kanisa kwa wafuasi wake wote wa kipagani.

Ili kujipatia uwezo, akazikubali desturi nyingi za ibada ya jua kutoka kwa wapagani wale. Maafikiano haya mengi ya kulegeza masharti, kama vile Krismasi na Ista(Easter) [Pasaka] yamekwisha kuelezwa. Nyingine katika desturi hizo ni uadhimishaji wa Jumapili. Ilionekana inafaa zaidi kuwaruhusu wapagani kuitunza siku yao wenyewe ya ibada katika siku ile ya Jumapili, na kuwaomba Wakristo kuungana nao katika kuitunza. Kwa hiyo, Konstantino ndiye hasa aliyeitoa amri ya kwanza ya kuitunza Jumapili badala ya Sabato. Mabaraza ya Kanisa la Kipapa yakaiimarisha sheria ile mpaka ikawa imeotesha mizizi kabisa katika Ukristo na Ulimwengu.

Ushuhuda Wa Historia

Tukigeukia sasa kwenye ushuhuda wa wanahistoria wa kidunia, unaweza kusoma ukweli wa mambo hayo wewe mwenyewe. Kila usemi umefafanuliwa wazi katika kumbukumbu za historia. Kutoka katika Encyclopedia Brittanica chini ya kichwa 'SUNDAY' tunasoma hivi: "Alikuwa ni Konstantino aliyetoa kwanza sheria ya utunzaji sahihi wa Jumapili, na ambaye ... aliagiza kwamba ingekuwa inasherehekewa daima katika Dola yote ya Kirumi." Hapa yapo maneno ya Dkt. Gilbert Murray, M.A., D.Litt., L.L.D., F.B.A., profesa wa Lugha ya Kigiriki katika Chuo Kikuu cha Oxford: "Sasa kwa vile Mithra (Mithras) alikuwa ni 'Jua, Asiyeshindikana,' na Jua lilikuwa ni 'Nyota ya Kifalme,' dini hiyo ikamtafuta mfalme ambaye ingemtumia kama mwakilishi wa Mithra hapa duniani... Mfalme wa Kirumi alionekana wazi kwamba ndiye aliyesondwa kidole kuwa mfalme wa kweli. Kinyume kabisa na Ukristo, Umithra (Mithraism) ulimtambua Kaisari kuwa ndiye mchukuzi wa Neema, na wafuasi wake walijaa katika majeshi na idara za Serikali... Ilikubalika sana [dini hiyo] hata ikaweza kuulazimisha ulimwengu wa Kikristo kuipokea siku yake ya jua (Sun-Day) badala ya Sabato, sikukuu yake ya kuzaliwa jua, tarehe ishirini na tano ya Desemba, kama ndiyo siku ya kuzaliwa Yesu." HISTORY OF CHRISTIANITY IN THE LIGHT OF MODERN KNOWLEDGE.

Dkt. William Frederick anasema ukweli ule ule wa historia: "Mataifa yalikuwa ni watu wenye kuabudu sanamu ambao waliliabudu jua, na Jumapili (Sunday) ilikuwa ndiyo siku yao takatifu sana. Sasa, ili kuwafikia watu katika nyanja hii [ya dini], linaonekana kuwa ni jambo la kawaida tu, na la lazima, kuifanya Jumapili kuwa siku ya mapumziko ya Kanisa. Wakati huu lilikuwa ni jambo la maana kwa Kanisa ama kuichagua siku ya Mataifa, ama kuwafanya Mataifa hao kubadili siku yao. Kuibadili siku ya Mataifa lingekuwa ni chukizo na kipingamizi kwao. Kwa kawaida Kanisa lingeweza kuwafikia vizuri zaidi [Mataifa wale] kwa kuitunza siku yao." SUNDAY AND CHRISTIAN SABBATH, uk. 169, 170.

Gazeti la North British Review linatoa sababu zifuatazo kwa kuichagua siku ya wapagani ya Jumapili (Sun-day): "Siku ile ile hasa ilikuwa ni siku ya jua (Sunday) ya majirani zao wapagani na wananchi kwa jumla, na uzalendo wao ukawaunganisha kwa furaha na kwa kuzingatia manufaa ya kuifanya [siku hiyo] pasipo kuchelewa kuwa siku yao ya Bwana na Sabato yao... Kanisa lile la zamani, kwa kweli, lilifungwa kwa kuichagua Jumapili ----- mpaka hapo ilipojizatiti na kuwa [siku] kuu kabisa, wakati ilipokuwa imechelewa mno kufanyiwa badiliko jingine." Gombo la XVIII, ukurasa 409.

Ukatoliki Unakiri

Kwa kuwa unabii wa Danieli ulitabiri kwamba Upapa unge"azimu" kubadili "majira na sheria" hebu na tuulize kama ulihusika na badiliko hilo la Sabato. Tunataka kufanya haki kwa kila mmoja, na kupata ushuhuda wa kweli kutoka kwa wote. Madondoo kadhaa yafuatayo yamechukuliwa kutoka kwa mamlaka zinazoaminika za Kikatoliki ambazo zinaeleza kwa wazi madai ya Upapa kuhusu jaribio hilo lililofanyika. Kutoka katika CATHOLIC ENCYCLOPEDIA, Gombo la IV, ukurasa 153, "Kanisa... baada ya kuibadili siku ya mapumziko kutoka Sabato ya Wayahudi, au siku ya saba ya juma, kwenda siku ya kwanza, likaifanya amri ya tatu kumaanisha Jumapili kuwa ndiyo siku itakayotakaswa kama Siku ya Bwana."

Gazeti la CATHOLIC PRESS, (Sydney, Australia) la Agosti 25, 1900 linalielezea jambo hilo kwa maneno haya: "Jumapili imewekwa na Wakatoliki, na madai yake ya kuitunza yanaweza kutetewa tu kwa kanuni za Kikatoliki... Tangu mwanzo wa Maandiko mpaka mwisho hakuna kifungu hata kimoja kinachoidhinisha uhamisho wa siku ya juma ya ibada kutoka siku ya mwisho ya juma kwenda ile ya kwanza." Gazeti la CATHOLIC MIRROR la Septemba 23, 1894 linaliweka suala hilo kwa njia hii: "Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya kuwako Mprotestanti, kwa nguvu ya utume wake, lilibadili siku toka Jumamosi kwenda Jumapili."

Hapa kuna semi kutoka katika Katekisimu mbili kuonyesha madai ambayo tunayajadili: Kutoka katika THE CONVERT'S CATECHISM OF CATHOLIC DOCTRINE, by Rev. Peter Geiermann,

"SWALI ----- Sabato ni siku gani?

"JIBU ----- Jumamosi ndiyo siku ya Sabato.

"SWALI ----- Kwa nini tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi?

"JIBU ---- Tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki, katika Baraza la Laodikia (336 B.K.) lilihamisha taratibu ya ibada kutoka Jumamosi kwenda Jumapili." ----Toleo la Pili, uk. 50.

Rev. Stephen Keenan katika DOCTRINAL CATECHISM yake anayo haya ya kusema:

"SWALI ----- Unayo njia nyingine yo yote ya kuthibitisha kwamba kanisa linao uwezo wa kuanzisha sikukuu ambazo zinashikwa kama amri?

"JIBU ----- Kama lisingekuwa na nguvu kama hizo, lisingaliweza kufanya kile ambacho wanadini wote wa siku hizi wanakubaliana nacho ----- lisingaliweza kuweka utunzaji wa Jumapili siku ya kwanza ya juma mahali pa utunzaji wa Jumamosi siku ya saba, badiliko ambalo halina Maandiko yo yote yanayolipa kibali hicho." ----- Ukurasa 174.

Tafadhali zingatia neno "kuweka mahali pa," usemi ambao tumeutumia tena na tena kuelezea shughuli za mamlaka hii.

Katika kitabu chake cha QUESTION BOX, uk.179, Kadinali Gibbons anatoa ungamo hili la kushangaza: "Iwapo Biblia ndiyo kiongozi peke yake kwa Mkristo, basi, Mwadventista wa Sabato ana HAKI kuitunza JUMAMOSI pamoja na Myahudi ... Je, si jambo la AJABU kwamba wale wanaoifanya Biblia kuwa MWALIMU WAO WA PEKEE, wangekuwa na kigeugeu hicho katika jambo hili kwa kufuata MAPOKEO ya Kanisa Katoliki?"

Mojawapo ya changamoto kuu kuliko zote ambayo imetupwa mbele ya Uprotestanti imo katika usemi wa Baba Enright, Rais wa Chuo cha Redemptor kule Marekani: "Lilikuwa ni Kanisa Takatifu la Katoliki lililobadili siku ya mapumziko toka Jumamosi kwenda Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Nalo halikuwalazimisha tu wote kuishika Jumapili, bali liliwashurutisha watu wote kufanya kazi siku ya saba chini ya tamko la adhabu ya laana (anathema). Waprotestanti ... wanadai kuwa na heshima kuu kwa Biblia, lakini kwa tendo lao hili la ibada la kuiadhimisha Jumapili, wanakiri kwamba Kanisa Katoliki lina uwezo [wa kubadili siku]. Biblia inasema, 'Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.' Walakini Kanisa Katoliki linasema, HAPANA: Itakase siku ya kwanza ya juma, na tazama, ulimwengu wote uliostaarabika unasujudu kwa kicho na kuitii amri hii ya Kanisa Takatifu la Katoliki."

Yakupasa wewe kuijibu changamoto hiyo! Utamtii nani? Sikiliza maneno haya ya C.F. Thomas, Katibu Mkuu wa Kadinali Gibbons akijibu barua inayohusu badiliko la Sabato: "Ni kweli Kanisa Katoliki linadai kwamba badiliko hilo lilikuwa kitendo chake. Na kitendo hicho ni ALAMA [MARK] ya uwezo na mamlaka ya Uongozi wa Kanisa [Katoliki] katika masuala ya kidini." Kwa hiyo mambo yanakuwa wazi ----- Mungu anasema kwamba Yeye ni Mungu wa kweli; ametupa Sabato kama Muhuri wa Mamlaka Yake kama Muumbaji wa vyote. Kwa kuitunza Sabato tunaitambua mamlaka Yake kama Mungu wa kweli. Walakini, Kanisa Katoliki linajitokeza na kusema kweli maneno kama haya: "Hapana, usiitakase Sabato; itakase siku ya kwanza ya juma [Jumapili]. Ni sisi tulioibadili, na badiliko hilo ni ALAMA ya uwezo wetu wa kutangua sheria na mamlaka ya Mungu."

Kwa hiyo, ALAMA YA MNYAMA ni JUMAPILI ya bandia ambayo kwayo mamlaka hii ya Mnyama inajitahidi kutaka itambuliwe kuwa ndiyo mamlaka iliyo kuu kuliko Muumbaji Mwenyewe. Alama, au Muhuri, ya Mamlaka ya Mungu [Sabato] imeondolewa na mahali pake imewekwa Alama ile [Jumapili] ambayo

Upapa unadai kuwa ni mamlaka yake. Laiti dunia yote ingaliweza kuliona kwa wazi jambo hili kuu sana lililo mbele yetu leo! Ni kwa nani sisi tutatoa UTII wetu ----- je! ni kwa Mungu au ni kwa Mnyama? Tunapoelewa mambo yalivyo hasa inatupasa kufanya UAMUZI mkubwa sana ama kuitunza Sabato ya kweli na kuitambua Mamlaka ya Mungu; ama kuipokea Sabato ya Uongo [Jumapili] na kuyatambua madai ya Kanisa Katoliki. Mwishowe inatupasa kupokea MUHURI WA MUNGU au ALAMA YA MNYAMA. Kuna pande mbili tu ----- MUNGU au JOKA, KWELI au UONGO, BIBLIA au MAPOKEO.

Kitabu kilichochapishwa mwaka 1956 chenye kichwa cha "THE FAITH OF MILLIONS" ambacho kinapatikana sasa katika Duka la Vitabu la Kikatoliki kama kitabu cha kiada (textbook) kuhusu dini hii ya Katoliki kina usemi huu wa kusisimua katika ukurasa wake wa 473: "Walakini, kwa vile Jumamosi, sio Jumapili, imetajwa kwa wazi katika Biblia, je! si ajabu kwamba wale wasio Wakatoliki wanaojidai kuichukua dini yao moja kwa moja kutoka katika Biblia na sio kutoka kwa Kanisa hili, wanaitunza Jumapili badala ya Jumamosi? Naam, kusema kweli, ni kukosa msimamo; walakini badiliko hilo lilifanyika karibu karne kumi na tano kabla ya kuzaliwa Uprotestanti, na kufikia wakati ule desturi hii [ya kuitunza Jumapili] ilikuwa inafuatwa ulimwenguni kote. [Waprotestanti] wameiendeleza desturi hii, japokuwa imejengwa juu ya mamlaka ya Kanisa Katoliki, wala sio juu ya fungu lo lote la Biblia linaloeleweka wazi. Uadhimishaji huo [wa Jumapili] unabaki kuwa kumbukumbu ya Kanisa Mama ambalo kutokana nalo madhehebu zisizokuwa za Kikatoliki zilijitenga mbali nalo ----- ni sawa na mvulana anayekimbia toka nyumbani kwao, lakini ambaye bado amechukua mfukoni mwake picha ya mama yake, ama msokoto wa nywele zake [mamake]."

Pamoja na [usemi] huo juu ongeza changamoto hii ya Kadinali Gibbons katika gazeti la CATHOLIC MIRROR la Desemba 23, 1893: "Haki na busara inataka tukubali moja au jingine kati ya mambo haya mawili ya kuchagua: aidha UPROTESTANTI NA KUITAKASA JUMAMOSI, au UKATOLIKI NA KUITAKASA JUMAPILI. Maafikiano kati ya mambo hayo mawili hayawezekani.

Waprotestanti Wanaafiki

Labda unashangaa kwamba Makanisa ya Kiprotestanti yanafikiri nini juu ya mambo haya ambayo tumekuwa tukiyatafakari. Watasema wao wenyewe. Hapa yapo MAUNGAMO ya kweli ya makanisa yale juu ya hoja hii ya Sabato. Semi zote zimedondolewa kutoka kwa wawakilishi wenye mamlaka kubwa sana [wa makanisa ya Kiprotestanti]. Hapa kuna dondoo kutoka kwa Dkt. Edward T. Hiscox, mwandishi wa Kanuni ya Kanisa la Kibaptisti, "Palikuwapo na bado ipo amri ya kuitakasa siku ya Sabato, lakini siku ile ya Sabato sio Jumapili. Walakini, itasemwa na kwa kuonyesha furaha kiasi fulani, ya kwamba Sabato ilihamishwa toka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya juma.... Ni wapi inapoweza kupatikana kumbukumbu ya kitendo kama hicho? Sio katika Agano Jipya ----- sio kabisa.... Ni kweli, mimi nami najua vema ya kwamba Jumapili ilianza kutumika mapema katika historia ya Kikristo kama siku ya dini, kama tunavyojifunza kwa Mababa Wakristo, na kutoka katika vianzo vinginevyo. Lakini NI JAMBO LA KUSIKITISHA JINSI GANI ya kwamba

inakuja ikiwa imetiwa ALAMA YA UPAGANI, na kubatizwa kwa jina la Mungu-jua, wakati ilipochaguliwa na kutumiwa na UASI ule wa Kipapa, na kurithishwa kama urithi mtakatifu kwa Uprotestanti!' (Imedondolewa kutokana na Karatasi la Mada iliyosomwa mbele ya Mkutano Mkuu wa Wachungaji mjini New York uliofanyika Novemba 13, 1893). Kiongozi huyu mkuu wa Kibaptisti anafanya muhtasari katika sentensi chache wa yale yote yaliyokwisha kusemwa katika kurasa za kijitabu hiki.

Gazeti la Kanisa la Presbyterian liitwalo "CHRISTIAN AT WORK" lilisema hivi: "Wengine wamejaribu kujenga hoja ya uadhimishaji wa Jumapili juu ya amri ya Mitume, wakati Mitume hao hawakutoa amri yo yote hata kidogo juu ya suala hilo.... Ukweli ni huu, mara tu tunapotumia Maandiko halisi ya Biblia, WASABATO wanayo hoja bora sana." Toleo la Aprili 19, 1883. Gazeti la METHODIST THEOLOGICAL COMPENDIUM linasema hivi: "Ni kweli kwamba hakuna amri yo yote ya hakika kwa ubatizo wa watoto wachanga.... Wala hakuna [amri yo yote] kwa kuitakasa siku ya kwanza ya juma."

Dkt. W.R. Dale (Kanisa la Congregational) katika kitabu chake cha "THE TEN COMMANDMENTS,' uk.106,107, asema, "Ni wazi ya kwamba haidhuru kwa ukali au kwa bidii jinsi gani tunaweza kuitunza Jumapili, HATUITAKASI SABATO. Sabato ilianzishwa kwa amri maalum ya Mungu. Hatuwezi kudai amri kama hiyo kwa utunzaji wa Jumapili.... Hakuna mstari hata mmoja katika Agano Jipya unaodokeza kwamba tunaweza kupata adhabu yo yote kwa kuvunja utakatifu unaodhaniwa tu wa Jumapili."

Msimamo wa KILUTHERI, kama ulivyofunuliwa katika kitabu chao cha Augsburg Confession of Faith, unasema, "Utunzaji wa Siku ya Bwana (Jumapili) haujajengwa juu ya amri yo yote ya Mungu, bali juu ya mamlaka ya Kanisa." Mwakilishi wa Kanisa la Episcopal aitwaye Neander anaandika hivi katika kitabu chake cha HISTORY OF THE CHRISTIAN RELIGION AND CHURCH, ukurasa 186: "Sikukuu ya Jumapili, kama sikukuu zingine, ilikuwa ni amri ya wanadamu, na ilikuwa mbali na makusudi ya Mitume wale kuweka amri ya Mungu kwa njia kama hii, ilikuwa mbali nao na mbali na Kanisa lile la mwanzo la Mitume kuhamisha kanuni za [utunzaji wa] Sabato kwenda Jumapili."

Katika kitabu kile cha TEN RULES FOR LIVING kilichoandikwa na Clovis G. Chappell, twasoma maneno haya: "Tungepaswa kukumbuka kwamba Sabato ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu. Ni kweli tunatambua kwamba Sabato yetu [Jumapili] sio ile inayotunzwa na Wayahudi. Yao ilikuwa ni siku ya saba ya juma, ambapo yetu ni siku ya kwanza. Sababu ya kuiadhimisha siku hii ya kwanza badala ya siku ile ya saba haina msingi wa amri yo yote [ya Mungu] iliyo dhahiri. Mmoja atayachunguza bure Maandiko ili kutafuta kibali cha kubadili [siku ya ibada] toka siku ya saba kwenda ile ya kwanza. Wakristo wale wa zamani walianza kuabudu katika siku ile ya kwanza ya juma kwa sababu Yesu alifufuka toka kwa wafu siku ile. Kadiri miaka ilivyopita, siku hii ya ibada ikafanywa kuwa siku ya mapumziko pia, sikukuu iliyoamriwa na Serikali. Jambo hilo lilitokea katika mwaka ule wa 321. Kwa hiyo, Sabato yetu ya Kikristo [Jumapili], haitokani na amri yo yote [ya Mungu] iliyo dhahiri." Ukurasa 61.

Alama Hii Italazimishwa

Tungeweza kuendelea kutoa semi kutoka kwa dazeni ya vianzo vya madhehebu mengine, lakini nafasi hairuhusu. Jibu lako ni lipi kwa mambo haya? Kwa wazi tumeona kwamba Mungu alitabiri kutokea kwa mamlaka ambayo ingejaribu kuibadili Sabato; historia inaandika ya kwamba mamlaka hiyo ilifanya jaribio hilo; mamlaka yenyewe inaungama kwamba ilijaribu kuibadili [Sabato]; na Waprotestanti nao wanaungama ya kwamba badiliko hilo lilifanyika. Ni wangapi watakaochukua msimamo wao upande wa Biblia?

Kwa kasi sana ulimwengu unaukaribia wakati ule SABATO itakapokuwa ni JARIBIO KUU [KIPIMO KIKUU] LA UTII. Madai yake yatawekwa mbele ya wakazi wote wa ulimwengu huu. Wakati ule, mambo yatakapowekwa wazi, mtu mmoja mmoja ataupokea MUHURI WA MUNGU au ALAMA YA MNYAMA. Kitabu cha Ufunuo kinaeleza juu ya TANGAZO LA AMRI YA MWISHO kutoka kwa Serikali [zote] za ulimwengu huu ambalo litataka KULAZIMISHA ALAMA HII [YA MNYAMA ----- JUMAPILI] juu ya ulimwengu WOTE. "Naye awafanya WOTE, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, WATIWE CHAPA [ALAMA] katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze KUNUNUA wala KUUZA, isipokuwa ana chapa [alama] ile, yaani, jina la Mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16,17.

Ni dhahiri kwamba hakuna aliyepata ALAMA hiyo [sasa] mpaka hapo ITAKAPOLAZIMISHWA JUU YA WATU WOTE kwa njia ya kupitishwa Bungeni kama Sheria ya Serikali za wanadamu. Hapo ndipo SABATO YA KWELI na JUMAPILI YA UONGO zitakapofunuliwa kwa wazi kabisa hata hakuna atakayekwepa kufanya UAMUZI ----- uamuzi wa KUITUNZA SABATO YA KWELI kwa moyo na mkono wake, au KUITII SABATO YA UONGO [JUMAPILI] YA PAPA. Katika sura inayofuata utajifunza jinsi ya kulitambua taifa litakaloiongoza dunia [yote] kuipokea Jumapili ya Uongo, na litakalotafuta kuilazimisha alama ile ya utii kwa Papa [Jumapili] kwa kutumia NGUVU [za dola].

IV. Marekani (U.S.A.) Katika Unabii

Mtu ye yote angejivunia kuwa Mmarekani. Kwa kweli hakuna sehemu yo yote duniani ambako watu wake wanaufurahia uhuru kamili kama katika nchi yetu ya Marekani (United States of America). Je, umepata kustaajabu kwa nini jambo hilo ni la kweli? Kuna sababu yake ya kutokea DEMOKRASIA katika sehemu hii ya dunia. Sio bahati nasibu tu kwamba Amerika ni mji mkuu wa uhuru katika ulimwengu mzima. Kwa kweli, Mamlaka ile ya Mnyama ya Ufunuo kumi na tatu ilihusika sana na kutokea kwa [taifa hili la] Amerika.

Unaweza kuwa unajiuliza mwenyewe, "Kwa vipi mamlaka hii ya Papa imehusika na kuwako kwa Marekani?" Ilikuwa ni kwa sababu ya MATESO ya Mamlaka hiyo ya Mnyama kule Ulaya [Magharibi] hata ikatokea Marekani. Mababa Wasafiri (Pilgrim Fathers), ili KUYAKWEPA MATESO ya kidini ya Papa, walikimbilia kwenye Ulimwengu Mpya wa Amerika ambako wangeweza kufuata DHAMIRI zao katika kumwabudu Mungu wao.

Hebu sasa na tupate picha kutoka kwenye kurasa za unabii katika Neno la Mungu. Mafungu kumi ya mwanzo ya Ufunuo kumi na tatu yanaeleza jinsi Upapa ulivyoanza na kutwaa mamlaka yake. Tumekwisha kujifunza tayari unabii huu kwa kinaganaga. Fungu lile la kumi linafunga kwa maelezo ya kukamatwa mateka [mahabusu] kwa Papa [Pius wa VI) katika mwaka ule wa 1798. "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga. Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu." Kisha mara hiyo Yohana akamwona mnyama yule wa pili katika maono yake, ambaye anamweleza katika fungu linalofuata. "Kisha nikaona mnyama mwingine akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo, akanena kama Joka." Ufunuo 13:11. Hebu na tuwe waangalifu sana katika kumtambulisha mnyama huyu wa pili. Kuna pointi kadhaa ambazo zitatufunulia utambulisho wa mamlaka hii.

KWANZA kabisa, anaonekana "akipanda juu" wakati ule ule Mnyama yule wa kwanza alipokuwa anapata jeraha lake la mauti. Kwa kuwa Mnyama yule wa kwanza (Upapa) alipata jeraha lake mwaka 1798 wakati Jenerali Berthier alipomkamata mahabusu Papa [Pius wa VI], basi, tungemtafuta mnyama huyu wa pili na kumwona akipanda juu wakati ule. Hii inamaanisha kwamba karibu na mwaka 1798 mamlaka hiyo ingekuwa inajitokeza ulimwenguni. PILI, mnyama huyu wa pili angepanda juu "kutoka katika NCHI." Huyo yuko kinyume na Mnyama yule wa kwanza ambaye alitoka MAJINI. Tuligundua katika Ufunuo 17:15 ya kwamba MAJI yaliwakilisha JAMAA na MATAIFA. Mnyama huyu wa pili, akipanda kutoka katika nchi, angeonyesha picha ya TAIFA likijitokeza katika sehemu fulani ya dunia ambako hakuna ustaarabu [watu] uliotangulia wala halaiki ya watu. Ukosefu wa maji huonyesha uchache wa watu.

TATU, TAIFA hili lilikuwa na pembe mbili kama mwana-kondoo, nazo hazikuwa na vilemba [taji] kama zile alizokuwa nazo Mnyama wa kwanza. Alipanda kwa amani, kama mwana-kondoo, na ule ukosefu wa taji [vilemba] huonyesha ya kwamba [taifa

hilo] halikuongozwa na wafalme. Halikuwa na utawala wa kifalme, wala utawala wa mabavu [udikteta]. Kila kitu kuhusiana na mnyama huyu kuonyesha utawala wa amani wa KIDEMOKRASIA.

Mnyama Wa Pili Atambulishwa

Sasa tuko tayari kumtambulisha mnyama huyu wa pili. Hakuna mashaka yo yote kuhusu utambulisho wake. Kuna taifa moja tu katika historia linalotimiza maelezo hayo. MAREKANI [THE UNITED STATES OF AMERICA] ndilo taifa peke yake lililokuwa "linapanda juu" kupokea mamlaka yake mwaka 1798, wakati Mnyama yule wa kwanza anapata jeraha lake la mauti. Katiba yake ilipitishwa kwa kura mwaka 1787, na Sheria ya Haki za Binadamu ilikubalika katika mwaka wa 1791. Pia, ilikuwa ni katika mwaka ule wa 1798 ambapo taifa la marekani kwa mara ya kwanza lilitambulikana kama ni mamlaka ya dunia. Wanahistoria wanaandika kwamba palikuwa na kitu fulani cha ajabu na cha kudra ya Mungu kuhusu kuinuka kwa nchi hii.

Kwa kutimiza kabisa unabii huu taifa hili lilitokea katika Ulimwengu Mpya, ambako kulikuwa hakuna ustaarabu uliotangulia. Lilikuja kwa amani, kwa njia ya kidemokrasia, na kujikita juu ya kanuni kuu mbili za UPROTESTANTI na SERIKALI YA JAMHURI. Kanisa na Serikali vikawa VIMETENGANISHWA. Babu zetu walikuwa wamechoshwa kuona maovu ya Serikali ile iliyounganisha DINI NA SERIKALI [UPAPA].

Hebu hapa na tusome usemi wa John Wesley, mwanafunzi wa ajabu wa Biblia, na mwasisi wa Kanisa la Methodisti. Akiandika panapo mwaka wa 1754 katika kitabu chake cha "New Testament with Explanatory Notes" baada ya kumfafanua Mnyama wa kwanza wa Ufunuo kumi na tatu kuwa alikuwa anauwakilisha UPAPA, alisema hivi: "Mnyama... mwingine ... Lakini huyo bado hajaja, ingawa hawezi kuwa mbali sana; kwa maana hana budi kutokea mwisho wa miezi arobaini na miwili [1798] ya Mnyama yule wa kwanza." Ukurasa 427. Zingatia, tafadhali, ya kwamba Wesley alikuwa anatazamia kuliona taifa kutokea katika kipindi kifupi sana ambacho kingekubaliana na maelezo ya unabii huu. Ni Marekani (U.S.A.) peke yake ingeweza kutimiza matarajio hayo.

Lingekuwa jambo jema kama tungekomea papa hapa katika utafiti wetu, lakini tusingeweza kuwa wakweli kwa Maandiko kama tusingesoma maelezo yaliyobaki ya unabii huu. Fungu la kumi na moja na la kumi na mbili yanaendelea kusema hivi, "naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo, akanena kama Joka. Naye atumia uwezo wote wa Mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie Mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona." Kwa maneno mengine, wakati ungekuja ambapo Marekani ingebadilisha sauti yake ya upole ya kidemokrasia. Chini ya mvuto fulani ingeanza KULAZIMISHA IBADA, "akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia Sanamu yule Mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Akapewa kutia pumzi katika ile SANAMU YA MNYAMA, hata ile Sanamu ya Mnyama INENE, na KUWAFANYA wote wasioisujudu Sanamu ya Mnyama WAUAWE. Naye awafanya

wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, WATIWE CHAPA [ALAMA] katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote ASIWEZE KUNUNUA WALA KUUZA, isipokuwa ana CHAPA [ALAMA] ile, yaani, jina la Mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:14-17.

Taifa [lo lote] linanena kwa njia ya Sheria zake. Huenda likaonekana kwetu kana kwamba ni jambo lisilosadikika tunaposoma mambo haya leo kwamba [taifa hili la] Marekani lingepata kushawishika kwa kupitisha sheria za dini, na kujaribu KUWALAZIMISHA watu kuabudu kwa mtindo fulani, walakini unabii kamwe haujakosa kutimia. Litaufanyia SANAMU Upapa, au litaanzisha MFUMO UNAOFANANA na mamlaka ile. DINI NA SERIKALI VITAUNGANISHWA pamoja kiasi cha kuweza kulazimisha sheria za dini na kwa njia hiyo litafanana na mfumo ule wa Upapa [wa kuvaa kofia mbili].

Kulingana na unabii huu Amerika mwishowe italazimisha ALAMA YA MNYAMA. Hii inamaanisha nini? Alama yenyewe ni kitu gani? Kwa msingi wa Neno la Mungu tumeonyesha ya kwamba itakuwa ni SABATO YA UONGO [JUMAPILI] ambayo ilianzishwa na Mamlaka ile ya Mnyama [Upapa]. Kule kuitunza Jumapili badala ya Sabato ile ya Biblia kunadaiwa na MAKASISI wake na VIONGOZI kuwa ni kuonyesha UTII kwa Kanisa Katoliki. Je, Marekani baadaye itataka kulazimisha utunzaji wa Jumapili? Hivyo ndivyo hasa mambo yanavyojionyesha sasa hivi katika siasa za Marekani.

Haidhuru tupende kiasi gani kusadiki vinginevyo, nchi yetu hii tuipendayo itaanza kutumia mamlaka yake kulazimisha utunzaji wa Jumapili. Tayari msingi umekwisha kuwekwa. Hivi sasa kila Jimbo (State), isipokuwa moja tu, lina SHERIA ZA JUMAPILI kama hizo katika vitabu vyao. Katika sehemu nyingine [za Majimbo hayo] sheria hizo za dini zimeleta shida kiuchumi kwa Wasabato. Miji mikuu michache imeshurutishwa KUWAKATAZA KUNUNUA AU KUUZA bidhaa zo zote [siku hiyo] kwa wale wanaokataa kuitunza Jumapili. Unabii wa Ufunuo 13:17 unaonyesha kuwa vizuio vya uchumi [kupiga marufuku] vitatumika, "tena kwamba mtu awaye yote ASIWEZE KUNUNUA WALA KUUZA, isipokuwa ana chapa [alama] ile."

Amri Ya Jumapili Kitaifa Iko Karibu

Mahakama Kuu ya Marekani (Supreme Court) imekataa kwamba sheria zile za Jumapili [za Majimbo] ni kinyume na KATIBA [ya nchi] ama zina UBAGUZI. Jambo hilo linafungua njia kwa sheria zile za Majimbo ambazo zinaleta utata na ziko kinyume ili ziweze KUBADILISHWA na kuwa SHERIA YA JUMAPILI moja kwa Taifa zima, ambayo itaweka MFUMO MMOJA NA KULAZIMISHA JUMAPILI katika nchi yote ya Amerika. Pamoja na hatua kubwa zinazochukuliwa kuruhusu udhibiti wa Serikali ya Muungano (Federal Control) juu ya uhuru wa mtu mmoja mmoja, hatua hii ya KURATIBU SIKU YA IBADA haitaonekana kuwa ni mapinduzi makubwa sana hapo itakapochukuliwa.

Zingatia haya vizuri: Kutokea kwa mambo hayo kuko upeoni [kumekaribia sana]. Wale wanaokataa kuipokea siku ya uongo ya ibada watakabiliwa na KUTOZWA FAINI, KUZUIWA KUNUNUA NA KUUZA, KIFUNGO, na mwishowe TISHIO LA KIFO. Suala hili la Sabato litakapofanywa hivyo kuwa suala la kitaifa, hapo ndipo watu watakapolazimishwa kukubali kusimama upande mmoja au mwingine. Alama ya Mnyama wakati huo itawekwa juu ya wote WATAKAOKATAA KUITII AMRI YA MUNGU inayowataka kuitakasa Siku ya Sabato. Kwa kuikubali Alama hii ya UTII KWA PAPA [Jumapili], wanaikataa Alama ambayo Mungu anadai kwamba ni ISHARA ya Mamlaka Yake ----- SABATO ya siku ya saba.

Kukata Shauri

Mmoja anaweza kutoa hoja hii, "Mambo hayo yote yananihusu nini mimi?" Hiyo ni hoja ya maana, na hata jibu lake ni la maana zaidi. Wokovu wako wa milele unategemea UAMUZI wako leo. Huwezi kuutupilia mbali unabii huu unaohusu UTII kwa amri hii ya Sabato. Hakuna hoja juu ya kufaa au kutokufaa kwake. Tunashughulika na Sheria ile ya AMRI KUMI ambayo iliandikwa na Mungu Mwenyewe. Kuvunja mojawapo ya amri hizo ni KUTENDA DHAMBI[Yakobo 2:10-12], na hakuna ye yote anayetenda dhambi kwa makusudi atakayeokolewa. Kuitunza Sabato ya siku ya saba ndicho KIPIMO CHA UTII NA UPENDO kwa Mungu. "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni DHAMBI." Yakobo 4:17.

Kwa kasi sana ulimwengu huu unajiunga chini [ya mojawapo] ya BENDERA hizo mbili. Wakati UMEKWISHA. Pambano Kuu linafikia hatua zake za mwisho. Wakati ekumenio (ecumenism) inalivuta kundi moja kubwa la madhehebu kuingia katika kambi lisilokuwa na mikazo yo yote ya imani, likiwa limejengwa kabisa juu ya UASI dhidi ya Sabato ya Sheria takatifu ya Mungu, kundi jingine linatambulishwa kuwa ni la wale "wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Jaribio hilo kadiri linavyozidi kuwa kali zaidi, ndivyo inavyompasa kila mtu mmoja mmoja KUCHAGUA KUMTII MUNGU au MAPOKEO, KUITUNZA SABATO YA KWELI au ILE YA UONGO [JUMAPILI], KUPOKEA MUHURI WA MUNGU, au ALAMA YA MNYAMA. Sasa ndio wakati wa kulimaliza jambo hili. "Heri wale wazishikao amri zake, wawe na haki kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake." Ufunuo 22:14 (Tafsiri ya Toleo la King James).